**Kigogo** CHADEMA asimulia siku nne za shida mahabusu

UKURASA 5



**Fisi** alivyokwepa risasi 49 baada ya kuua mtoto

UKURASA 8




UKURASA 11


# Nipashe

Jumatano Julai 28, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580655


MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# CHANJO CORONA RASMI




**RAIS** Samia kuchanjwa leo, Zanzibar mguu sawa, UVCCM wataka Askofu Gwajima achukuliwe hatua... *Endelea ukurasa 2, 3 & 17*



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi akivishwa Tuzo ya Juu ya Heshima ya "LEGION d" HONNER" na Balozi wa Ufaransa hapa nchini, Frederic Clavier, aliyotunukiwa na Rais wa Jamhuri ya Ufaransa, Emmanuel Macron, katika hafla iliyofanyika Ikulu, jijini Zanzibar jana. **Habari kamili uk. 7**. **PICHA: IKULU**

UKURASA WA 7

## RAIS SAMIA ATAJA HATIMA TOZO ZA MIAMALA YA SIMU

RAIS Samia amesema serikali kesho itatoa uamuzi kuhusu hatima ya tozo za miamala ya simu baada ya kupokea ripoti ya kamati iliyoundwa.

Aliyasema hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam alipoapisha mabalozi 13 aliowateua...

## BoT sasa yapunguza riba mikopo ya benki

UKURASA 3

## Shahidi amtaja JPM kesi ya kina Sabaya



UKURASA 2

**MICHEZO** SIMBA: HATUJAPATA OFA YA MIQUISSONE UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Chanjo corona sasa rasmi

**Na Mary Geofrey**

RAIS Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuzindua mpango wa chanjo ya corona (UVIKO 19) leo Ikulu jijini Dar es Salaam na baadaye kuanza kutolewa katika ngazi ya mkoa nchini.

Mkuu wa nchi anaongoza mpango huo katika mikakati ya kujikinga na ugonjwa wa UVIKO 19 ambao umeshaua watu zaidi ya milioni nne duniani kote.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alitangaza uzinduzi huo wa chanjo jana mkoani humo alipozungumza na waandishi wa habari.

Alisema tukio hilo litarushwa mbashara na vyombo vya habari na kwamba baada ya Rais kuchanjwa, wakuu wa mikoa nao wataanza kuzindua katika maeneo yao nchini.

Dk. Dorothy alisema katika utoaji wa chanjo hiyo wanazingatia makundi yote ya vipaumbele wakiwamo watu wenye umri kuanzia miaka 50, wenye magonjwa sugu, watoa huduma za afya na wanaofanya kazi katika mazingira hatarishi ya kupata maambukizi.

"Kutokana na kuwa dozi ambazo serikali imepokea kwa awamu ya kwanza ni milioni 1.058, hivyo tutaanza kuchanja makundi ya kipaumbele kwenye kila mkoa kama ilivyoainishwa kwenye mwongozo," alisema.

Sambamba na hilo, waziri huyo alisema wizara yake inatarajia kuanza kutoa vipindi vya elimu kwa umma kuhusu uchanjaji na wananchi watapata fursa ya kuuliza maswali na kujibiwa.

"Wizara tunaamini kuwa kupitia elimu tuna ufafanuzi wa hoja kwa misingi ya kisayansi ndio wananchi watapata ufahamu sahihi kwa ajili ya wao kuamua kwa hiari bila malipo kupata huduma hii itakayowaweka salama," alisema.

Hadi sasa, jumla ya watu 29 wameripotiwa kupoteza maisha nchini katika wimbi la tatu la UVIKO 19 na wengine zaidi ya 680 wakiripotiwa kuugua ugonjwa huo.

Waziri huyo alisema serikali imeweka wazi malengo yake ni kutoa chanjo hiyo inayoanza kutolewa leo kwa Watanzania milioni 35 sawa na asilimia 60.

**WAZIRI MKUU**

Wakati huo Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema serikali haijamlazimisha na wala haitamlazimisha mwananchi kuchanjwa, hivyo Watanzania wapuuze upotoshaji unaosambazwa kupitia mitandao ya kijamii.

"Hakuna aliyelazimishwa kuchanja chanjo hiyo na wala hakuna mahali palipoandikwa kwamba lazima wananchi wachanjwe. Chanjo ni hiari tusipotoshane kwa sababu hakuna serikali inayoweza kuandaa mpango wa kuwaangamiza wananchi wake."

Aliyasema hayo jana alipozungumza na wananchi wa Wilaya ya Ruangwa kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kijiji cha Nandagala, akisisitiza waendelee kuchukua tahadhari na kujikinga na UVIKO 19.

Majaliwa alisema serikali imeleta chanjo hiyo ili kutoa fursa kwa Watanzania watakaohitaji kuchanjwa kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa wa UVIKO 19, waweze kuipata kwa ukaribu na urahisi zaidi na si vinginevyo.



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Mkurugenzi wa Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC) barani Afrika, Dk. John Nkengasong, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Shahidi amtaja JPM kesi ya kina Sabaya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

SHAHIDI wa sita wa Upande wa Jamhuri, Bakari Raibu Msangi (38), ametoa ushahidi mahakamani akidai aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya (34) katika tuhuma za kuvamia duka la Mohamed Saad na kupora baadhi ya vitu na mali, lilikuwa agizo la Hayati Dk. John Magufuli.

Shahidi huyo ambaye ni Diwani wa Sombetini jijini Arusha (CCM), alidai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Odira Amworo, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha.

Msangi alidai kuwa alipofika katika duka la Saad, alimkuta Sabaya kwenye duka hilo na kwamba mshtakiwa huyo alihoji sababu za diwani huyo kuwatetea watu aliowaita wahujumu uchumi.

Shahidi huyo alidai Ole Sabaya alimweleza kuwa alikwenda dukani huko kwa agizo la Hayati Rais Magufuli, kwa kuwa wamiliki wa duka hilo walikuwa wanafanya biashara kinyume cha sheria.

"Sabaya aliniambia kuwa mimi nawatetea wahalifu ambao ni wahujumu uchumi, watakatishaji wa fedha na wanafanya biashara bila ya kutoa risiti, najaribu kumzuia wakati ameagizwa na Rais John Magufuli," alidai Msangi.

Shahidi huyo pia alidai aliwekwa chini ya ulinzi na Sabaya kisha kuporwa fedha kiasi Sh. 390,000.

Mbali na Ole Sabaya, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Silvester Nyegu (26) na Daniel Mbura (38), wote wakikabiliwa na kesi ya jinai namba 105, yenye mashtaka matatu ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Shahidi huyo wa sita alidai mahakamani huko kuwa ni mfanyabiashara anayefanya shughuli zake katika Mtaa wa Pangani, Kata ya Kati na ni mkazi wa Kata ya Sombetini jijini Arusha.

Akihojiwa na Wakili Mkuu wa Serikali, Tumaini Kweka, shahidi huyo alidai mbali na shughuli ya biashara, yeye ni mwanasiasa na Diwani wa Sombeni.

Msangi alidai kuwa Februari 9, mwaka huu, akiwa katika majukumu yake ya kikazi, majira ya saa 11:30 jioni, alipigiwa simu Ali Saad Hajirini.

Alidai aliambiwa Ole Sabaya alikuwa dukani kwa kaka yake (Mohamed Saad) na amewapiga sana watu waliokuwa dukani huko. "Nilimwambia nitakwenda kuangalia kuna tatizo gani kwa kuwa Sabaya namfahamu na nilipofika karibu na duka hilo niliona watu wengi wakiwa wanashangaa kinachoendelea dukani.

"Kulikuwa na watu wawili hapo nje ya duka wanaonifahamu, mmoja alinitahadharisha nisiende huko kwa kuwa nitakufa kwa kuwa Sabaya yupo huko anapiga watu, nilimjibu 'ngoja niende, acha aniue'.

"Nilipofika karibu na hilo duka, niliwakuta watu wawili wameshika bastola na wamejifunika kwa kofia kufunika sehemu za macho na uso, niligonga mlango wa geti mara tatu haukufunguliwa. Kwa kuwa ulikuwa umerudishiwa nusu niliufungua na kuingia ndani," alidai.

Shahidi huyo alidai kuwa alipoingia ndani, watu wawili waliokuwa wameshika bastola, walifunga mlango kwa nje na alipoingia ndani ya duka alikuta mtu mmoja amewekwa chini ya ulinzi kwa kulazwa kifudifudi sakafuni.

Alidai kuwa kutoka geti la kuingilia hadi dukani, ndani kuna umbali kama wa mita sita na kuna taa kubwa ambazo zilikuwa zimewashwa.

"Niliposogea karibu na kaunta, nilikuta kundi la watu wengi wamesimama hapo, akiwamo Sabaya, msaidizi wake Silvester Nyengu, dada mmoja mwenye lafudhi ya kikenya alikuwa amepigishwa magoti na wengine sikuweza kuwatambua na walikuwa kama watu 10.

"Pia wengine niliowatambua ni Hajirini, Numan na mtu mwingine mmoja ambaye sikumtambua, walikuwa wamelazwa chini na mimi nilimsogelea Sabaya, alikuwa ameshika mkanda wa kiunoni nikamsalimia nikamwambia 'Sabaya habari yako' mara tatu lakini hakuitikia.

"Alikuwa akijitutumua kwa kupandisha mabega juu na mmoja wa walinzi wake waliniambia 'kwani hufahamu jina la mkuu?'" Alidai.

Shahidi huyo alidai kuwa baada ya kukataliwa salamu, Sabaya aliwaambia walinzi wake wamweleze jina lake kwamba anaitwa General Lengai Ole Sabaya na anapomsalimia anapaswa kuonyesha utii.

"Nilitii agizo kwa kumwita General Lengai Ole Sabaya, hapo aliridhika na kufurahia sana huku akijipiga kifua akisema naam naam na aliitikia kwa kunguruma huku akijitengeneza.

"Muda siyo mrefu kupita aliniuliza kwamba nimefuata nini hapo dukani huku akisema nimekwenda kuwatetea Answary wenzangu na nilimjibu kwamba nilikwenda kufahamu ndugu zake wana shida gani," alidai.

Alidai kuwa baada ya hapo alihoji sababu ya Sabaya kutoka wilayani kwake (Hai) kwenda kufanya kitendo hicho Arusha wakati Arusha kuna viongozi na mamlaza za kiserikali ikiwamo polisi, TRA na TAKUKURU.

Alidai baada ya kumwambia maneno hayo, Sabaya alikasirika sana na wakati akijitengenezea aliona bastola kiunoni na wakati huo walinzi wake walikuwa tayari wameshamzunguka kila kona.

"Wakati General Sabaya alipokuwa amechukia, walinzi wake walinizunguka aliwaagiza wanisachi (kupekua), na baada ya hapo walinipiga kipigo kizito," alidai na kuongeza kuwa aliporwa Sh. 390,000 na simu ya mkononi.

"Nilimwomba Sabaya asiniue kwa kuwa mke na mtoto wangu walikuwa ni wagonjwa, alinijibu hata kama anafahamiana na mdogo wangu (Juma Raibu), kiherehere changu ndiyo kimeniponza kwa kwenda pale,

"Baada ya kipigo kizito aliagiza walinzi wake wanifunge pingu mikononi na miguuni huku wakiendelea kunipiga nikiwa nimeegemea kaunta hadi nilipoteza fahamu na baada ya muda nilipata fahamu na nilipoamka nilimwomba maji mmoja wa walinzi kwa kuwa nilihisi kifo, lakini Sabaya aliagiza nisipewe maji huku akiniambia nisifuatilie mambo yake," alidai.

# UVCCM yamvaa Gwajima, yataka achukuliwe hatua

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UMOJA wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM), umesema hawaungi mkono kauli ya Mbunge wa Kawe, Josephat Gwajima, kuhusiana na chanjo ya corona na kukishauri chama hicho kimchukulie hatua za kinidhamu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dodoma, Katibu Mkuu wa Umoja huo, Kenani Kihongosi, alisema maneno yaliyotolewa na Gwajima ni ya kichochezi na yanayo mwelekeo wa kuwagawa wananchi.

Pia alisema kitendo hicho ni utovu wa nidhamu kwa kuwa serikali imeshatoa msimamo kuwa chanjo itatolewa kwa hiari.

Kihongosi alisema umoja huo unalaani na kupinga vikali kauli ya Gwajima na kumtaka kama ana hoja aipeleke kwenye vikao halali vya chama vilivyopo kwa mujibu wa Katiba.

"Maneno aliyotoa ni ya kichochezi kwa kuwa Rais na serikali ilishatoa msimamo wananchi wapate chanjo. Yeye amesema chanjo haifai ina madhara, tumuulize yeye amesomea? Yeye ni daktari? Ni utovu wa nidhamu kwa kuwa msimamo wa serikali ni kuwakinga wananchi," alisema.

Kwa mujibu wa Kihongosi, utaratibu wa CCM kama mbunge ana hoja, kina vikao huku akiwaomba viongozi wa dini wajielekeze kwenye mahubiri yanayosaidia wananchi.

"Lazima atambue dhamana aliyonayo amepewa na CCM na sisi vijana wa CCM tunalaani vikali kauli zile na viongozi wa namna hii wachukuliwe hatua," alisema.

Kihongosi alitoa rai kwa viongozi wa serikali na chama wenye tabia ya kuzungumza vitu kwenye vyombo vya habari bali watumie vikao halali vilivyopo kufikisha hoja zao.

Alisema umoja huo unasimama na Rais Samia Suluhu Hassan na serikali katika suala la chanjo na kuwahimiza Watanzania kwenda kupata chanjo hiyo kwa hiari.

Alisisitiza Watanzania kufuata maelekezo yanayotolewa na wataalam wa afya katika kujikinga na corona kwa kuhakikisha wananawa mikono mara kwa mara kwa maji tiririka na kuvaa barakoa.



Mwenyekiti wa Taasisi ya vyombo vya habari Kusini mwa Afrika (MISA-TAN), Tawi la Tanzania, Salome Kitomari, akitoa mafunzo kwa waandishi wa habari kutoka mikoa mbalimbali mjini Morogoro jana, kuhusu kuzingatia miiko na maadili ya taaluma yao, wakati wa kuandika habari zinazohusu milipuko wa virusi vya corona, ili kuepuka kuleta taharuki. **PICHA: MARCO MADUHU**

# BoT yalegeza masharti riba mikopo benki

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imelegeza masharti ya usajili wa mawakala wa benki kwa kuweka sharti la kuwa na Kitambulisho cha Taifa (NIDA) badala ya uzoefu wa biashara kwa miezi 18, ili kuongeza fedha katika taasisi za fedha kutokana na ongezeko la amana na kupunguza riba za mikopo.

Pia, Benki Kuu imeanzisha mfuko maalum wenye thamani ya Sh. trilioni moja ambao utatumika kukopesha benki na taasisi za fedha kwa riba ya asilimia tatu ili zikopeshe sekta binafsi.

Uamuzi huo ni miongoni mwa hatua tano za kisera zilizoamuliwa na benki hiyo zinazolenga kuweka msukumo wa kuongeza kasi ya mikopo kwa sekta binafsi na kupunguza riba na utekelezaji wake umeanza jana.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Gavana wa BoT, Prof. Florens Luoga, alitaja hatua zingine ni kupunguza kiwango cha sehemu ya amana za benki kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu, ukomo wa riba kwenye akaunti za kampuni za watoa huduma za fedha kwa njia ya simu za mkononi na kupunguza kiwango cha mtaji kinachotakiwa kuwekwa na benki za biashara kwa ajili ya kutoa mikopo.

Alisema benki hiyo imeondoa sharti la uzoefu wa kufanya biashara kwa angalau miezi 18 kwa waombaji wa biashara ya wakala wa benki badala yake waombaji wa biashara hiyo watatakiwa kuwa na Kitambulisho cha Taifa au namba ya kitambulisho.

Kadhalika, alisema Benki Kuu imetoa unafuu kwa benki za biashara kwa kupunguza kiwango cha kisheria cha amana ambacho benki na taasisi za fedha zinatakiwa kuweka benki kuu ikiwa ni sehemu ya kutekeleza sera ya fedha.

Nafuu hiyo itatolewa kwa benki itakayotoa mikopo kwa sekta kilimo kulingana na kiasi cha mkopo kitakachotolewa.

"Benki itakayonufaika itatakiwa kutoa mikopo kwa sekta ya kilimo kwa riba isiyozidi asilimia 10 kwa mwaka hatua hii inalenga kuongeza mikopo katika sekta ya kilimo na kupunguza riba katika mikopo inayotolewa," alisema.

Kuhusu ukomo wa riba, Prof. Luoga alisema Benki Kuu imeweka ukomo wa kiwango cha riba kinachotolewa na benki za biashara kwenye akaunti za kampuni zinazotoa huduma ya fedha kwa njia ya simu za mkononi na riba itakayotolewa kwenye akaunti hizo haitazidi riba itolewayo na benki husika katika amana za akiba na wanalenga kupunguza gharama za upatikanaji wa fedha kwa benki zinazokopesha.

Akizungumzia kuhusu mfuko maalum, alisema Benki Kuu imeanzisha mfuko huo na benki au taasisi ya fedha itakayofaidika itatakiwa kukopesha sekta binafsi kwa riba isiyozidi asilimia 10 kwa mwaka na kuongeza ukwasi na kupunguza riba za mikopo kwa sekta binafsi.

Alifafanua kuwa hatua ya tano Benki hiyo imepunguza kiwango cha mtaji kinachotakiwa kuwekwa na benki za biashara kwa ajili ya kutoa mkopo na itasaidia kutoa fursa kwa benki hizo kutoa mikopo zaidi kwa sekta binafsi kuliko ilivyokuwa awali.

Prof. Luoga alisema hatua hizo zimechukuliwa kwa mujibu wa Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, sura 197 na Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, sura ya 437, Benki Kuu itatoa mwongozo wa namna ya utekelezaji wa hatua hizo kwa benki, taasisi za fedha na kampuni zinazotoa huduma za fedha kwa njia ya simu za mkononi.

"Pamoja na hatua hizi, Benki Kuu inaziagiza benki za biashara na taasisi za fedha kuweka na kutekeleza mikakati ya kupunguza riba za mikopo na kuhamasisha upatikanaji wa amana," alisema.

Awali, alisema janga la Uviko-19 limeathiri shughuli za kiuchumi kutokana na nchi zinazofanya biashara na Tanzania kuchukua hatua, kudhibiti kuenea ikiwamo vizuizi vya kusafiri.

Alisema, serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kupunguza athari za janga hilo ili kuchochea ukuaji wa uchumi.

"Pamoja na hatua hizo kasi ya ukuaji wa uchumi ilipungua hadi kufikia asilimia 4.8 kwa mwaka 2020 kutoka asilimia saba kwa mwaka uliotangulia, ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi pia ulipungua na kufikia ukuaji wa kati ya asilimia 2.3 hadi 9.1, viwango vya riba kwa mikopo inayotozwa na benki za biashara vimeendelea kuwa juu kwa wastani wa asilimia 17 licha ya ongezeko la ukwasi na hatua zingine zilizochukuliwa," alisema.


NMB
Karibu yako

**TAARIFA KWA WATEJA**

Mpendwa Mteja,

Benki yako ya NMB inapenda kukutaarifu kuhusu mabadiliko ya baadhi ya Makato katika huduma zake zifuatazo, kuanzia tarehe **28/08/2021;**

**Tanzanite Debit MasterCard**

| Aina ya Ada | Ada Mpya (TZS) |
|---|---|
| Ada ya Utoaji | 5,900/- |
| Ada ya Kadi ya Mwaka | 14,000/- |

Kwa maelezo zaidi tafadhaili wasiliana nasi kupitia namba 0800 002 002 au kwa barua pepe: tuambie@nmbbank.co.tz

***Imetolewa na Utawala wa NMB Bank Plc.***

216375902

www.nmbbank.co.tz

## TANGAZO

# International Commercial Bank (Tanzania) Limited.

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 30.06.2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO MWAKA ILIYOPITA |
|---|---|---|---|
| | | 30.06.2021 | 31.03.2021 |
| A. | *MALI* | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 1,080 | 927 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 15,177 | 3,986 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 7,278 | 8,294 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 4,299 | 2,439 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 34 | (3) |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 34,879 | 36,314 |
| 12 | Mali Nyingine | 9,853 | 9,473 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,149 | 1,126 |
| 16 | **JUMLA YA MALI** | **73,748** | **62,555** |
| B. | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 0 | 500 |
| 18 | Amana za Wateja | 44,643 | 33,092 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 162 | 162 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 73 | 73 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,198 | 1,113 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 62 | 62 |
| 27 | Dhima Nyingine | 3,051 | 2,968 |
| 28 | Madeni | - | - |
| **29** | ***JUMLA YA DHIMA*** | **49,189** | **37,969** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** ***(16 kutoa 29)*** | **24,559** | **24,586** |
| C. | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 29,975 | 28,940 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 7,639 | 7,455 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (11,539) | (11,319) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (1,516) | (490) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | - | - |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| 37 | ***JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA*** | **24,559** | **24,586** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 1,176 | 1,229 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 21,021 | 20,444 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 2,837 | 2,499 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| D. | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 33.3% | 39.3% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 50.7% | 50.2% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 92.5% | 124.2% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 55.2% | 67.0% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 63.0% | 75.2% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 32.7% | -10.1% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 17.9% | -6.7% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 30.06.2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO MWAKA LINGANISHI LA MWAKA ULIOPITA | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA | LIMBIKIZO LINGANISHI LA MWAKA ULIOPITA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 30.06.2021 | 30.06.2020 | 30.06.2021 | 30.06.2020 |
| 1 | Mapato ya Riba | 1,019 | 1,475 | 2,093 | 3,214 |
| 2 | Gharama za Riba | 428 | 804 | 851 | 1,501 |
| 3 | Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2) | ***591*** | ***671*** | ***1,242*** | ***1,713*** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | - | 2 | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 338 | 632 | 338 | 661 |
| 6 | **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **105** | **250** | **266** | **646** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 12 | 20 | 20 | 83 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 24 | 48 | 58 | 98 |
| | 6.3 Gawio | - | | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 69 | 182 | 188 | 466 |
| 7 | **Gharama Zisizo za Riba:** | **1,385** | **1,360** | **2,684** | **2,749** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 565 | 564 | 1,170 | 1,181 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 113 | 49 | 126 | 66 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 707 | 746 | 1,388 | 1,502 |
| 8 | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(1,026)** | **(1,071)** | **(1,516)** | **(1,051)** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | - | - | - | - |
| 10 | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(1,026)** | **(1,071)** | **(1,516)** | **(1,051)** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - | - | - |
| 12 | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(1,026)** | **(1,071)** | **(1,516)** | **(1,051)** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 58 | 60 | 58 | 60 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | (51) | (53) | (76) | (52) |
| 15 | Mapato kwa Hisa zilizochujwa | (51) | (53) | (76) | (52) |
| 16 | **Idadi ya Matawi** | 4 | 5 | 4 | 5 |
| | ***BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI*** | | | | |
| 1 | Uwiano wa Faida kabla ya kodi na Wastani wa mali | -6.0% | -5.5% | -4.3% | -2.7% |
| 2 | Uwiano wa Faida baada ya kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -16.7% | -22.2% | -12.2% | -10.9% |
| 3 | Uwiano wa matumizi yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 123.1% | 78.8% | 113.8% | 71.2% |
| 4 | Uwiano wa mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali zinazozalisha | 5.1% | 6.1% | 5.1% | 8.4% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA WA MWAKA ULIOISHIA 30.06.2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | ROBO MWAKA YA SASA | ROBO MWAKA ILIYOPITA | LIMBIKIZO LA MWAKA WA SASA | LIMBIKIZO LINGANISHI LA MWAKA ULIOPITA |
|---|---|---|---|---|---|
| | | 30.06.2021 | 31.03.2021 | 30.06.2021 | 30.06.2020 |
| I | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | (1,026) | (490) | (1,516) | (1,051) |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | | | | |
| | - Hasara Katika Mali | 404 | 64 | 468 | 872 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 1,097 | (584) | 513 | 6,740 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 11,051 | (3,780) | 7,272 | 6,121 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | - | - | - | - |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 168 | (231) | (63) | 1,042 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (380) | 282 | (98) | (2,734) |
| | - Kodi Iliyolipwa | - | - | - | - |
| | -SMR | 56 | 267 | 323 | |
| | - Mengineyo | (36) | - | (36) | 1,569 |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | ***11,335*** | ***(4,471)*** | ***6,864*** | ***12,559*** |
| II | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | | | |
| | Gawio Lililopokewa | - | - | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | (90) | (755) | (844) | (53) |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | | | - | - |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | (2,045) | 4,783 | 2,738 | (3,340) |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(2,135)** | **4,029** | **1,894** | **(3,393)** |
| III | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 1,035 | - | 1,035 | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - | - | - |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | **1,035** | **-** | **1,035** | **-** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **10,235** | **(442)** | **9,793** | **9,166** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Mwaka/Mwaka | 8,311 | 8,753 | 8,753 | 48,062 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Mwaka/Mwaka | **18,546** | **8,311** | **18,546** | **57,228** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 30.06.2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| Mwaka wa sasa | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo (bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2021** | **28,940** | **-** | **(11,320)** | **7,455** | | **-** | **25,076** |
| Marekebisho ya mwaka uliopita | | | (36) | - | | | **(36)** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | | (1,516) | | | | **(1,516)** |
| | | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | |
| Miamala na wanahisa | | | | | | | |
| Gawio lililolipwa | | | | | | | |
| Ziada ya Kisheria | | | | | | | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | | | | | | |
| Mengineyo | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| Nyongeza ya Mtaji | 1,035 | | | | | | 1,035 |
| **Salio la mwisho wa kipindi 30.06.2021** | **29,975** | **-** | **(12,872)** | **7,455** | **-** | **-** | **24,559** |
| | | | | | | | |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2020** | **20,025** | **-** | **(4,086)** | **4,140** | | **-** | **20,079** |
| Marekebisho ya mwaka uliopita | | | (109) | | | | (109) |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | | | (3,809) | | | | (3,809) |
| | | | | | | | |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | | | | | | | |
| Miamala na wanahisa | | | | | | | |
| Gawio lililolipwa | | | | | | | |
| Ziada ya Kisheria | | | (3,315) | 3,315 | | | |
| Tengo la Ziada ya Jumla | | | | | | | |
| Mengineyo | | | | | | | |
| | | | | | | | |
| Nyongeza ya Mtaji | 8,915 | | | | | | 8,915 |
| **Salio la mwisho wa kipindi 31.12.2020** | **28,940** | **-** | **(11,320)** | **7,455** | | **-** | **25,076** |

**Katika kuandaa taarifa hizi za fedha, sera za uandaaji ni zile zile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita.**

**Saini:**

**VILLY VELLAYAPPAN**
Ofisa Mtendaji Mkuu
Tarehe: 20 Julai 2021

**GEORGE MSAMBAZI**
Mkuu wa Fedha
Tarehe: 20 Julai 2021

**JOHN MWAKASONDA**
Mkaguzi Mkuu wa Ndani
Tarehe: 20 Julai 2021

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi,tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006,na zinaonesha hali halisi.

**Saini:**

**ALFRED MKOMBO**
Mjumbe wa Bodi
Tarehe: 20 Julai 2021

**HASHIMAH BINTI ISMAIL**
Mjumbe wa Bodi
Tarehe: 20 Julai 2021

216376702

# Kigogo CHADEMA asimulia siku nne za shida mahabusu

**Na Richard Makore,**
MWANZA

VIONGOZI na wanachama wa Chama Cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wamesimulia madhila waliyopitia kwa siku 4 walipokuwa mahabusu katika vituo vya polisi jijini Mwanza. Kadhalika, makada hao wamesimulia namna walivyodakwa hotelini usiku mnene na watu waliokuwa wamevalia kininja bila kujitambulisha ni kina nani.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Mwanza, Mjumbe wa Kamati Kuu ya CHADEMA, John Heche, alisema walikosa chakula cha kutosha na kwa wakati na walilala sakafuni kwenye chumba kimoja chenye upana wa mita 3.

Heche alisema katika chumba kimoja walikuwa mahabusi zaidi ya 60 na kwamba aliwakuta baadhi yao wakiwa wamekaa huko kati ya siku 48 hadi 60 bila kufikishwa kortini.

Alisema baadaye walikuwa wanakula vyakula walivyokuwa wakipelekewa na wanachama wa CHADEMA. Alisema kwa siku 4 walitukanwa, walidhalilishwa, kupekuliwa majumbani mwao na wengine walifungwa vitambaa vyeusi na kupandishwa gari wakati wanasafirishwa kutoka eneo moja hadi lingine.

Alisema sheria inamtaka askari akitaka kumkamata mtu ambaye siyo jambazi kama yeye kujitambulisha kwamba yeye ni nani na kumwambia kosa analomkamatia.

Alisema siku waliyokamatwa walitoka nyumbani kwa mmoja wa wanachama aliyewakaribisha viongozi hao akiwamo mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe.

Heche alisema baada ya kutoka kwa mwanachama huyo walimsindikiza Mbowe hotelini kwake, na kwamba wakati anarudi nyumbani kwake, ndipo watu waliovalia kininja walipovamia gari lake na kuanza kulipiga kwa kitako cha bunduki, huku wakimtaka ashuke chini.

# Wafanyabiashara Kariakoo walipwa bima ya mil. 438/-

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB kupitia Kampuni ya Reliance Insurance, zimewalipa bima ya Sh. milioni 438.4 wafanyabiashara 12 waliokata bima mbalimbali, kati ya walioungul iwa moto maduka yao katika Soko la Kariakoo, Julai 10, mwaka huu.

Hafla ya kuwakabidhi wafanyabiashara hao hundi yenye thamani hiyo, ilifanyika jana katika Ofisi za NMB Kariakoo Business Center, ambako waathirika hao walikiri kuwa hasara na maumivu yao ya kuunguliwa yamepozwa na malipo hayo ya haraka ya bima.

Akizungumza kabla ya kuwakabidhi hundi ya mfano, Mkuu wa Kitengo cha Bima Benki ya NMB, Martin Massawe, alitoa wito kwa Watanzania kujenga utamaduni chanya wa kuzilinda kwa bima mali na pesa wanazotafuta kwa jasho lao ili kuepuka maumivu yasiyo na mfariji wakati wa majanga.

"Tuko hapa kwa ajili ya kuwafuta machozi wafanyabiashara waliokata bima nasi kupitia mikopo yao ama waliokuwa na bima za mali bila mikopo, ambao walikuwa sehemu ya wahanga wa moto wa Julai 10, sokoni Kariakoo.

"Wito kwa Watanzania, moto wa Soko la Kariakoo uwe fundisho kwao juu ya umuhimu wa bima. Moto ama majanga huja bila kuyatarajia, unapokata bima unakuwa umejiwekea kinga kuilinda pesa ama mali uliyotafuta kwa jasho lako.

"Uwapo wa bima hukurejeshea nguvu haraka kana kwamba hakuna janga lililokutokea. Wito huu sio tu kwa bima za mikopo, bali mali zote kwani gharama za bima hizi ni nafuu mno," alisema Massawe mbele ya waathirika hao 12, ambao ni miongoni mwa waathirika wa moto sokoni Kariakoo.

Akisisitiza umuhimu na unafuu wa bima hizo, Massawe alitolea mfano wa bima ya moto kuwa hukatwa asilimia 0.25 ya thamani ya mali na kwamba kama mali ya Sh. milioni 100, makato yake ya bima ni Sh. 225,000 tu bila V.A.T kiasi ambacho ni rahisi kuliko bima za magari.

"Nyumba ya thamani ya Sh. Mil. 100, makato yake ya bima ni Sh. 150,000, sawa na 177,000 pamoja na V.A.T, hapa utaona ni kwa namna gani bima hizi ni nafuu, lakini zinazobeba nguvu kubwa majanga yanapotokea," alisema Massawe, na kuongeza kuwa moto ulipotokea walikuwa wa kwanza kukimbilia ili kujua hasara za wateja wao.

Joel Mwakalebela, Meneja Madai wa Kampuni ya Reliance Insurance, aliwapongeza waathirika hao kwa uamuzi wao wa kukata bima, huku akisisitiza Watanzania kutosubiri mikopo ili kukata bima, badala yake watumie huduma hizo ili kujilinda na majanga.

"Tukio la moto Kariakoo litufundishe kuwa bima sio tu ni kwa ajili ya pesa za mikopo, nenda kakate bima za moto, magari, nyumba, afya, mali na nyinginezo, kwa sababu majanga hayaepukiki, na pia yanapokuja hayapigi hodi kwetu."

Emmanuel Mbise, mmiliki wa maduka namba 019 na 026 yaliyoteketea kwa moto, alifichua kuwa maumivu waliyoyapata waathirika wa tukio hilo ni makubwa, lakini malipo ya bima kutoka NMB, yanawapa hafueni na faraja kubwa.

Naye Sajida Kagasheki, alisema amepata faraja kubwa kupitia malipo hayo ya bima, huku akiwataka Watanzania kukimbilia sana huduma za bima, ambazo ni mkombozi na mfariji wa kweli wakati wa matatizo kama ya moto, vifo, ulemavu, upotevu na kadhalika.

## International Commercial Bank (Tanzania) Limited.

### DISCLOSURE MADE UNDER REGULATION 11 OF BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATION, 2014

### MINIMUM DISCLOSURE OF BANK CHARGES AND FEES AS AT 30th JUN 2021

| SN | DESCRIPTION | TZS | USD | EURO | GBP |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | **MONTHLY MEINTENANCY FEE** | | | | |
| | ICB Savings Account | 2,000 | 1.5 | 1.5 | 1.5 |
| | ICB Salary Account | 2,000 | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Staff Savings Account | Free | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Current Account -Personal | 10,000 | 5 | 5 | 5 |
| | ICB Premier Current Account | 20,000 | 10 | 15 | 15 |
| | ICB Premier Savings Account | 20,000 | 10 | 15 | 15 |
| | ICB Current Account - Corporate | 15,000 | 7 | 7 | 7 |
| | Al-Wadiyah Savings Account | Free | Free | Free | Free |
| 2 | **MINIMUM OPENING BALANCE** | | | | |
| | ICB Savings Account | 20,000 | 50 | 50 | 50 |
| | ICB Salary Account | - | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Staff Savings Account | Free | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Current Account -Personal | 50,000 | 50 | 50 | 50 |
| | ICB Premier Current Account | 1,000,000 | 500 | 500 | 500 |
| | ICB Premier Savings Account | 1,000,000 | 500 | 500 | 500 |
| | ICB Current Account - Corporate | 100,000 | 100 | 100 | 100 |
| | Al-Wadiyah Savings Accounts | 20,000 | N/A | N/A | N/A |
| 3 | **MINIMUM OPERATING BALANCE** | | | | |
| | ICB Savings Account | 5,000 | 100 | 100 | 100 |
| | ICB Salary Account | 5,000 | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Staff Savings Account | 250 | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Current Account -Personal | 50,000 | 0 | 0 | 0 |
| | ICB Premier Current Account | 1,000,000 | 500 | 500 | 500 |
| | ICB Premier Savings Account | 500,000 | 500 | 500 | 500 |
| | ICB Current Account - Corporate | 50,000 | 0 | 0 | 0 |
| | Al-Wadiyah Savings Accounts | 5,000 | N/A | N/A | N/A |
| 4 | **EXTRA CHARGE ON TRN BELOW MINIMUM BALANCE** | | | | |
| | ICB Savings Account | 600 | 1.2 | 1.2 | 1.2 |
| | ICB Salary Account | 600 | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Staff Savings Account | N/A | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Current Account -Personal | 600 | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Premier Current Account | 5,000 | 1.2 | 1.2 | 1.2 |
| | ICB Premier Savings Account | 5,000 | N/A | N/A | N/A |
| | ICB Current Account - Corporate | 5,000 | N/A | N/A | N/A |
| | Al-Wadiyah Savings Accounts | N/A | N/A | N/A | N/A |
| 5 | **CASH WITHDRAW FEES** | | | | |
| | Cash withdraw at the counter (All Current accounts): Daily limits | Up to TZS 5Mil - 2000 , Above TZS 5Mil charge 0.13% Max TZS170,000 | 0.25% of the Amount | 0.25% of the Amount | 0.25% of the Amount |
| | Cash withdraw at the counter (All Savings accounts except ICB Chuo and Lenga Account): Daily limits | Up to TZS 5Mil - 1500 , Above TZS 5Mil charge 0.13% Max TZS 170,000 | 0.25% of the Amount | 0.25% of the Amount | 0.25% of the Amount |
| | premature withdrawal and withdraw more than 3 per quarter | 1% charge of the principal amount | 1% charge of the principal amount | 1% charge of the principal amount | 1% charge of the principal amount |
| 6 | **FUND TRANSFERS/REMITTANCES** | | | | |
| | Internal Transfers within ICB Bank | Free | Free | Free | Free |
| | Cross border transfers (TT, SWIFT) - outward | N/A | USD 50 (If charges are shared), | | |
| | Cross border transfers (TT, SWIFT) - outward | N/A | USD 70 (If all charges are born by sender) | | |
| | Inward Transfers (TT, SWIFT) | Free | USD 11.8 | | |
| | Amendment of TISS, SWIFT Message | 11,800 | USD 11.8 | | |
| | Amendment of TT, SWIFT Message | N/A | USD 20 | | |
| | TISS | 11,800 | USD 11.8 | | |
| | EFT (Bulk Payments): Out& Inward/salary processing fee | 3,000 per transaction | USD 2 per transaction | | |
| | Stop Payments (TISS/EFT/SWIFT) | 20,000 | USD 20 | | |
| 7 | **CASH DEPOSIT** | | | | |
| | ICB Accounts | Free | Free | Free | Free |
| | ICB Agency Banking | Free | N/A | N/A | N/A |
| | Bulk Cash | Free | Free | Free | Free |
| | Deposit of Coins | 0.1% of the Amount | N/A | N/A | N/A |
| | Small Denomination (1, 5, 10, and 20) | N/A | 5% of the Amount | 5% of the Amount | 5% of the Amount |
| 8 | **BALANCE ENQUIRY /STATEMENT** | | | | |
| | ICB ATM Balance Enquiry | free | N/A | N/A | N/A |
| | Balance Enquiry Within Banking Hall | free | Free | Free | Free |
| | interim statement | 1000 per page | 1 per page | 1 per page | 1 per page |
| | Monthly statement & E-statement | Free | Free | Free | Free |
| 9 | **CHEQUE DEPOSIT** | | | | |
| | Cheque From other Banks | Free | Free | Free | Free |
| | Outward Special Clearance – Local Settlement | 53,100 | 52.8 | 46 | 39.5 |
| | Inward Clearing | 1,000 | Equivalent to TZS | Equivalent to TZS | Equivalent to TZS |
| | Unpaid Cheque (Refer to drawer) | 35,000 | 20 | 20 | 20 |
| | Unpaid Cheque (Refer to drawer) | 50,000 | 1.5% Min 59 Max 118 | 1.5% Min 59 Max 118 | 1.5% Min 59 Max 118 |
| 10 | **CHEQUE BOOK** | | | | |
| | Cheque Book 100 Leaves | 100,000 | 50 | 50 | 50 |
| | Cheque Book 50 Leaves | 50,000 | 25 | 25 | 25 |
| | Stop payment order per leaf; Reported Lost/Stolen Cheque Book/leaf (per notice) | 35,000 | 23.6 | 17.7 | 17.7 |
| 11 | **BANKERS CHEQUE** | | | | |
| | Commission per issued Cheque | 30,000 | 23.6 | 17.7 | 17.7 |
| | Cancellation of Banker's cheque | 30,000 | 23.6 | 17.7 | 17.7 |
| 12 | **STANDING INSTRUCTIONS** | | | | |
| | SI - Set up/Amendment/closure | Free | Free | Free | Free |
| | SI-Execution per Entry within ICB | Free | Free | Free | Free |
| | SI-Execution per Entry outside ICB | 20,000 | 10 | 10 | 10 |
| | Unpaid SI due to Insufficient funds | Free | Free | Free | Free |
| 13 | **ATM/ DEBIT CARDS** | | | | |
| | **ATM Card issuance fee** | | | | |
| | PESAXPRESS CARD | 10,000 | NA | NA | NA |
| | **ATM Card replacement fee** | | | | |
| | PESAXPRESS CARD | 10,000 | NA | NA | NA |
| | **ATM Transaction fee** | | | | |
| | ATM card activation | Free | | | |
| | Blocking/Hotting ATM card | Free | | | |
| | Cash Withdrawal | 1,300 | N/A | N/A | N/A |
| | Intrabank Fund Transfer | 1,300 | N/A | N/A | N/A |
| 14 | **GENERAL ACCOUNT OPERATIONS** | **TZS** | **USD** | **EURO** | **GBP** |
| | Confirmation of Balance and Audit Statement | 50,000 | 25 | 25 | 25 |
| | Salary processing manually per entry | 3,000 | N/A | N/A | N/A |
| | Salary / Bulk payments through Online Banking | 10,000 | | | |
| | Advisory service - charged per advice | 2,500 | Equivalent to TZS | Equivalent to TZS | Equivalent to TZS |
| | Vouchers - Information less than one year | 15,000 | Equivalent to TZS | Equivalent to TZS | Equivalent to TZS |
| | Salary Alert per message | 118 | N/A | N/A | N/A |
| | Dormant Account Activation fee (all current Accounts) | 10,000 | 5 | 5 | 5 |
| | Court Order Closing of Account | Free | Free | Free | Free |
| | Deliberate closing of corporate account (within six months) | 20,000 | 10 | 10 | 10 |
| | Deliberate closing of Personal account (within six months) | 10,000 | 5 | 5 | 5 |
| | **Cash Change** | | | | |
| | Cash Coins per bag of TZS 100,000 | 2000 | N/A | N/A | N/A |
| 15 | **BONDS & GUARANTEE** | | | | |
| | Issuance of Bid Bond - Cash cover | 0.5% per Quarter | | | |
| | Issuance of Bid Bond - Other Security | 1.42% Per Quarter | | | |
| | Performance Bond-Cash Cover | 0.5% per Quarter | | | |
| | Performance Bond-Other security | 1.42% Per Quarter | | | |
| | Extensions | 1.42% Per Quarter | | | |
| | Amendments | Simple amendments$50 | | | |
| | Cancellations of Returned guarantees | Free | | | |
| | Cancellations of guarantees if not Returned | 20000 | | | |
| 16 | **ADVANCED PAYMENT GUARANTEE** | | | | |
| | Issuance - Cash cover | 0.5% Min 100,000 | | | |
| | Issuance - Security | 1.42% Min100,000 | | | |
| | **Import Collections (IC)-Inward Foreign Doc & Bills for Collections** | | | | |
| | Handling Commissions | 0.5% MinUSD100 | | | |
| | Correspondence swift charges | USD 50 | | | |
| | **Export Collections (EC)- Outward Foreign Doc & Bills for Collections** | | | | |
| | Handling Commissions | 0.5% MinUSD100 | | | |
| | Correspondence Commission-per tracer | USD 50 | | | |
| | Courier Charges | USD100 | | | |
| 17 | **CASA INTEREST RATE** | **TZS** | **USD** | **EURO** | **GBP** |
| | ICB Savings Account | 3% pa | 1.5% pa | 1.5% pa | 1.5% pa |
| | ICB Salary Account | 3% pa | 1.5% pa | 1.5% pa | 1.5% pa |
| | ICB Current Account -Personal | 0% pa | | | |
| | ICB Premier Current Account | 1.5% pa | | | |
| | ICB Premier Savings Account | 5% pa | | | |
| | ICB Current Account - Corporate | 0% pa | | | |
| | Al-Wadiyah Savings Account | 0% pa | 0.00% | - | - |

We, the undersigned have examined the above information and hereby declare that the information is true and correct to the best of our knowledge and information.

**Name:**

| | | |
|---|---|---|
| Villy Vellayappan | Chief Executive Officer | 20.07.2021 |
| George Msambazi | Head of Finance | 20.07.2021 |
| John Mwakasonda | Head of Internal Audit | 20.07.2021 |

216376702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Usalama wa chakula sasa uwe kipaumbele

**LEO** mkutano wa awali wa Umoja wa Mataifa kujadili mifumo salama ya kuzalisha chakula duniani, unahitimishwa, jijini Roma Italia ukiwa umeangazia mambo mbalimbali yanayohusu usalama wa chakula.

Katika mkutano huo mnyororo mzima wa kuzalisha chakula kuanzia mazao shambani, mifugo, samaki majini, hadi usaafirishaji, usindikaji, uhifadhi hadi kufikishwa mezani kuliwa unaangaziwa.

UN inaliona suala la usalama wa chakula na kuwapo lishe bora kwa kile kinacholiwa kuwa msingi wa kufanikisha Malengo 17 ya Maendeleo (SDGs), mojawapo ikiwa ni kuwezesha kila mtu kuwa salama.

Kimsingi, kinachoguswa hapa ni miongoni mwa malengo ya SGDs, hasa lile linaloangazia zaidi upande wa afya, ili kuhakikisha kila mtu anakuwa na afya bora.

Nasi tunakubaliana na mipango ya UN kwamba ipo haja ya kuhakikisha usalama katika chakula ili kulinda afya za Watanzania badala ya kuwapo mianya inayochangia baadhi ya watu kuhatarisha afya za wenzao.

Tunakubaliana na kile ambacho kinafanywa na UN, kwani kitasaidia watu kuzingatia afya kuanzia uzalishaji wa chakula, mazao shambani, mifugo, samaki, hadi usafirishaji, usindikaji, uhifadhi hadi kufikishwa mezani kuliwa.

Kwa nchini, kumekuwapo na taarifa kuwa, baadhi ya wakulima wakiwamo wa bustani hasa mboga, ambao hudaiwa kumwagilia maji ambayo si salama yakiwamo majitaka, hali ambayo ni hatari kwa afya za walaji.

Wakati hao wakifanya hivyo, hata waandaji wa vyakula vya kuuza wakiwamo mama lishe na baba lishe, nao hudaiwa kuweka hamira kwenye ugali ili wateja washibe kwa kiasi kidogo cha ugali.

Kwa upande mwingine, wauza supu na pweza, hudaiwa kuweka viagra, huku wale wanaokaanga chips wakidaiwa kutumia mafuta ya transfoma, lakini maziwa kuchanganywa na maji, unga wa ngano, ili kupata mtindi mzito.

Sisi tunaona ni wakati mwafaka kuwapo kwa mkutano, huo kwa ajili ya kusaidia dunia kutambua umuhimu wa ubora wa chakula na kuachana na mtindo huo tulioutaja ambao ni hatari kwa afya.

Kwa hapa nchini, tunashauri mamlaka kufuatilia kwa karibu taarifa za kuwapo kwa baadhi ya watu kuweka katika mazao au kuandaa vyakula katika mazingira hatarishi na kuchukua hatua za kisheria.

Tunaamini kwamba hatua zikichukuliwa, zikiwamo za kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa afya bora, usalama wa chakula utakuwapo kuanzia mashambani hadi nyumbani kinapoandaliwa hadi mezani kinapoliwa.

Hatua hiyo inaweza kusaidia wahusika kufanya shughuli zao kwa kuzingatia afya zao na za wateja wao kwa kuepuka kuweka hamira kwenye chakula, kuweka viagra au kukaangia mafuta ya transfoma.

Bila kufanya hivyo, afya za watu wengi zitakuwa hatarini na matokeo yake ni baadaye kuathiri nguvu kazi ya taifa pamoja na kuwa na taifa la watu wasiokuwa na mchango katika uzalishaji na uchumi kwa ujumla.

Tunashauri kwamba sisi kama taifa tusikubali watu wachache wenye maslahi binafsi kulifanyia mzaha suala la usalama wa chakula. Hivyo, Tanzania ikiwa mwanachama wa UN, ichukue hatua madhubuti za kuwalinda wananchi wake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Mtazamo wangu kauli ya Mbunge Gwajima

Na Sabato Kasika

**CCM** imeahidi kufuatilia kwa makini mienendo na kauli za baadhi ya wanachama wake ambao imedai wanapotosha umma na kwenda kinyume na maelekezo ya Mwenyekiti Rais Samia Suluhu Hassan, na pia maadili ya chama chao.

Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, anaeleza kuwa hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya wanaotumia nafasi hiyo kusukuma ajenda binafsi.

Anatoa kauli hiyo baada ya mbunge wa Kawe (CCM) na Askofu wa Kanisa la Ufufuo na Uzima, Josephat Gwajima, kudai daktari atakaye 'shadadia' chanjo ya corona bila kufanya utafiti wa kina kujua madhara ya muda mrefu na mfupi atakufa.

Ni katika ibada ya Jumapili iliyopita wakati akihubiri kanisani hapo ndipo alipoonyesha mashaka kuwa chanjo za corona zinaweza kuwa hatari kwa maisha.

Pengine si sahihi kama mbunge wa CCM kupingana na serikali yake hali ambayo inaweza kusababisha watu kukosa upande wa kusimamia kuhusu chanjo.

Askofu Gwajima ana ushawishi kwenye kanisa na jamii pia, hivyo kauli yake inaweza kuchukuliwa kwa uzito na pengine kusababisha wengi kutowaamini na kuwa na hofu na wanaopigia chapuo dawa hizo wakiwamo wakuu wa serikali.

Rais na Mwenyekiti wa CCM Taifa ndiye aliyekubali chanjo ya corona iletwe nchini, hivyo kusema kuwa wanaopigia chapuo dawa hizo wamepewa pesa, ni kama kumgombanisha na wananchi.

Huenda mbunge na Askofu Gwajima, akawa ameteleza kidogo kwa kauli hiyo, ambayo inapingana na juhudi za serikali za kukabiliana na corona.

Hata hivyo suala la COVID-19, limeibua mambo mengi na hasa taarifa feki, kujenga hofu na kuogopesha watu kuhusu chanjo yake.

Ndiyo maana Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Tedros Adhanom Ghebreyesus, anasema tangu kuzuka maradhi hayo, wanapambana na maadui wawili, taarifa feki pamoja na mlipuko wa COVID-19.

Anasema kumekuwapo na elimu nyingi zisizotokana na wataalamu wa afya ambazo dunia (wakiwamo Watanzania) wamekuwa wakipokea zinazidi kuwaweka njiapanda washindwe kujua ukweli au uongo uko wapi.

Pengine pia Gwajima ametumia maelekezo ya Mwenyekiti wa CCM, alipohutubia bunge na kuwataka wakosoe serikali na kuleta mambo chanya na mbadala kwa maendeleo.

Hata hivyo, katika vita hiyo vya corona ni vyema Rais, Wizara ya Afya na CCM wakatoa mwongozo unaohusu namna bora ya kutoa taarifa ili kuepusha uwezekano wa kuwa na maelekezo yanayokinzana na yenye kuwachanganya wananchi.

Kwenye suala la chanjo ya corona, busara itumika zaidi kwani wananchi wanaona ni jambo jipya, lakini kuna taarifa nyingi zinazotolewa na pia madhara yake yameelezwa kuwa ni pamoja na damu kuganda, kubadilisha mifumo ya nasaba (DNA) inayohusisha kinga na kwamba unaweza kuchanjwa lakini ukaumwa tena COVID-19 hata kupoteza maisha.

Waziri wa Afya wa Uingereza, Sajid Javid, alithibitisha kuambukizwa corona licha ya kuchanja mara mbili, lakini anaamini kuwa imesaidia kupunguza makali ya ugonjwa huo na sasa yuko salama, yote hayo ni mambo yanayoongeza tafakari ya chanjo.

Hivyo CCM badala ya kusema inafuatilia kauli za viongozi wake, ingependeza iwapo angeitwa na kusikilizwa, kwani inawezekana kupata maelezo mengine zaidi na serikali ikawa katika nafasi nzuri ya kuyafanyia ufafanuzi.

Pamoja na hayo ni vyema kiongozi huyo wa kiroho atumie muda mwingi kuhamasisha wananchi na waumini wake kuzingatia mwongozo wa Wizara ya Afya wa kujikinga na COVID-19.

Wizara imetoa mwongozo mpya wa karibuni unaeleza mambo mbalimbali kama kuvaa barakoa kwenye mikusanyiko, kunawa na kutumia vitakasa mikono.

# Dk. Mwinyi atunukiwa nishani ya juu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ametunukiwa Tuzo ya Juu ya Heshima inayofahamika kama "Legion d' Honner" na Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron, kutokana na mchango wake wakati akiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.

Dk. Mwinyi alitunukiwa tuzo hiyo jana na Balozi wa Ufaransa nchini Tanzania, Frederic Clavier, kwa niaba ya Rais Macron katika hafla iliyofanyika Ikulu, Zanzibar.

Kutokana na tuzo hiyo, Dk. Mwinyi alimshukuru Rais Macron kwa kuthamini mchango wake alioutoa wakati akiwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa miaka 10.

Alisema amepokea tuzo hiyo ambayo ni heshima kubwa kwa kuwa hutolewa kwa watu mbalimbali kutokana na mchango wao kwa nchi zao.

Dk. Mwinyi alisema katika kipindi cha miaka 10 akiwa Waziri, Tanzania ilishiriki katika operesheni tano za kudumisha amani barani Afrika.

Alisema serikali anayoiongoza iko tayari kushirikiana na wafanyabiashara wa Ufaransa ili kuleta maendeleo kwa wananchi wa Unguja na Pemba.

Pia alisisitiza kwamba amani na utulivu vilivyoko Zanzibar ni matokeo ya mazungumzo kati ya vyama vya siasa ambavyo viliamua kuunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa ili kuleta amani na maendeleo ya haraka.

Alisema kwa kuwa Ufaransa iko tayari kufanya kazi na Zanzibar, ana matumaini kwamba malengo ya maendeleo ya Zanzibar yatafikiwa kwa haraka.

Naye Balozi Clavier alisema kuanzia mwaka 2008 hadi 2012 na kuanzia mwaka 2014, Dk. Mwinyi alianzisha uhusiano wa karibu kati ya Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na Ufaransa.

Balozi Clavier alisema Rais Mwinyi alikuwa kiungo kilicholeta uhai katika ushirikiano wa nchi mbili hizo.

# Samia ataja hatima tozo miamala ya simu

**Na Enock Charles**

RAIS Samia (pichani) amesema serikali kesho itatoa uamuzi kuhusu hatima ya tozo za miamala ya simu baada ya kupokea ripoti ya kamati iliyoundwa.

Mkuu wa nchi aliyasema hayo jana Ikulu jijini Dar es Salaam alipoapisha mabalozi 13 aliowateua hivi karibuni.

Alisema serikali itaangalia namna bora ya kuboresha tozo hizo ili kupunguza malalamiko kwa wananchi, japo lengo kubwa la tozo hizo ni kujenga miundombinu ya barabara za vijijini ili kuwasaidia wakulima.

Vilevile, Rais Samia alisema kutokana na kukua kwa kilimo katika sehemu mbalimbali nchini, serikali imedhamiria kuimarisha miundombinu ya barabara ambazo nyingi ni mbovu na pia kuboresha miundombinu ya maji.

"Niwaambie Watanzania tumesikia vilio, tunakwenda kuangalia njia nzuri ya kwenda na hili lakini nataka niseme zipo ila tutaangalia njia nzuri ambayo haitaumiza watu. Serikali ipate na maendeleo tupate, kazi iendelee.

"Tunatarajia kupokea maoni ya Kamati tuliyoiunda tarehe 29 ambayo ni kesho kutwa (kesho) na baada ya hapo tutajulisha umma tunakwendaje kwenye hili, nachotaka kusema makato haya tuliyaweka kwa nia njema tu," alifafanua.

Katika hafla hiyo, Rais aliwataka mabalozi kutafuta fursa za kiuchumi, utalii na masomo kwa wanafunzi kutoka Tanzania, akisisitiza zipo fursa za masomo huwa zinajitokeza lakini walengwa hawazifikii, akitolea mfano fursa za masomo katika Jumuiya ya Madola.

"Sekta tunazotakiwa kuziangaza ni pamoja na sekta za utalii, biashara, uwekezaji, uchumi wa kidijitali na uchumi wa bluu. Mfano utalii kuna mikutano, kuandaa matamasha watalii kuja kuangalia utalii wetu, pia fursa za masomo," alisema.

Rais Samia pia aliitaka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kufanya haraka kupitia Sera ya Mambo ya Nje ili kubadili baadhi ya vipengele vilivyopitwa na wakati, hasa kwenye diplomasia ya uchumi na utamaduni wa Tanzania.



Kuhusu kupanda kwa bei ya mbolea, Rais Samia alisema serikali inatarajia kujenga kiwanda cha mbolea Dodoma ili kupunguza makali ya kupanda kwa bei ya bidhaa hiyo ambayo imeathiriwa na soko la dunia.

# Wamiliki leseni madini wakalia kuti kavu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TUME ya Madini imetishia kuwafikisha mahakamani wamiliki 443 wa leseni za utafutaji madini wanaodaiwa malimbikizo ya ada kiasi cha Sh. bilioni 9.31 ikiwa watashindwa kulipa ndani ya siku 60.

Mwenyekiti wa Tume hiyo, Prof. Idris Kikula, alibainisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kuhusu kuimarisha mfumo wa utoaji na usimamizi wa leseni za madini.

Alisema hadi juzi leseni hizo zilikuwa zinadaiwa kiasi hicho cha fedha zilizotokana na malimbikizo ya ada za mwaka tangu zilipotolewa.

"Wasipolipa ndani ya siku hizo, hatua za kisheria zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kufuta leseni hizo na wahusika kufikishwa mahakamani. Ikumbukwe kuwa lengo la serikali si kufuta leseni za wawekezaji bali ni kuhakikisha sheria, kanuni na taratibu zote zilizowekwa na nchi zinafuatwa na kutekelezwa," alisema.

Pia aliwaagiza maofisa madini wote nchini kufuta leseni zote ambazo hazijaendelezwa na ambazo hazijalipiwa ada ya mwaka kwa mujibu wa Sheria ya Madini Sura 123 baada ya siku 60, kuanzia tarehe ya tangazo hilo.

"Ndugu waandishi wa habari orodha ya leseni zote ambazo hazijaendelezwa na ambazo hazijalipiwa ada ya mwaka zinapatikana kupitia tovuti ya madini," alisema Prof. Kikula.

Pia alisema tume hiyo imeendelea kuongeza kasi ya utoaji wa leseni kwa kuimarisha mfumo wa utoaji na usimamizi wa leseni za madini.

"Kutokana na kasi hiyo, Tume ya Madini imeendelea kuwa na mwenendo chanya katika utoaji wa leseni za madini. Mwaka 2018/19 zilitolewa leseni 5,094, mwaka 2019/20 leseni 7,214 na mwaka 2020/21 zilitolewa leseni 7,862. Takwimu hizi zinathibitisha ukuwaji wa sekta ya madini nchini," alisema Prof. Kikula.

Pia alisema kuna baadhi ya kampuni na watu binafsi walioaminiwa na serikali na kupewa leseni wameshindwa kutekeleza masharti ya leseni kwa mujibu wa Sheria ya Madini ikiwa ni pamoja na kulipa ada ya leseni na kuziendeleza.

"Waziri wa Madini, Dotto Biteko, katika nyakati tofauti ameendelea kuielekeza Tume ya Madini na kuwahamasisha wawekezaji kuhakikisha wanaendeleza maeneo yao na kulipa ada stahiki za leseni zao," alisisitiza.

Pia alisema lengo la Waziri Biteko ni kuhakikisha kuwa wawekezaji wanapatiwa taarifa za ziada mapema kabla ya hatua za kisheria hazijachukuliwa.

"Nawasihi wawekezaji wote nchini kuhakikisha wanafuata maelekezo ya waziri na viongozi wengine wa serikali wakati wote," alisisitiza.


**THE ASSOCIATION OF PRIVATE HEALTH FACILITIES IN TANZANIA (APHFTA) LAKE ZONE**

**CAREER OPPORTUNITIES**

**APHFTA - LAKE ZONE DRIVER – 1 POSITION**

The Association of Private Health Facilities in Tanzania (APHFTA), Lake Zone, is seeking to recruit a Driver for the APHFTA Lake Zone office in Mwanza.

**Job Description**

**Reports to : Zonal Cordinator**
**Department : Finance and Administration**
**Supervisory role : None**
**Location : APHFTA LZ-Mwanza**

**Responsibilities:**
The drivers roles and responsibilities will be to drive office vehicles for the transport of authorized personnel, Collect and deliver mail, and other communications from and to the post office, government agencies and other institutions; Responsible for the day-to-day maintenance of the assigned vehicle, check oil, water, battery, brakes, tyres etc., performs minor repairs and arranges for other repairs to ensure that the vehicle is kept clean; Logs all trips, daily mileage, gas consumption, oil changes, greasing etc; Ensures that in the event of an accident, APHFTA rules/policies and traffic regulations are followed.

**Desired qualifications/Competencies:**
- A minimum of 'O' level pass;
- VETA OR NIT Certificate
- A valid driving licence B,C,D,E;
- A minimum of 3 years experience in a busy office especially in the NGO set up
- Age range from 25 years to 50 years
- Be fluent in Kiswahili Language, written and oral
- Cautious with defensive driving skills;
- Presentable with excellent interpersonal skills;
- Must be a person with initiative and high moral integrity;
- A good team player;

**Ready to work for long hours;**
**Applying Instructions**

**How to Apply**
If you believe you can demonstrate your abilities to meet the relevant criteria for this position, please submit your application letter with a detailed CV stating your current position, academic qualifications and skills with E-mail and telephone contacts, including names and contacts of 3 referees.

***Women/Girls are highly encouraged to apply.***

To be considered, your application must be received by 4th August 2021 addressed to:

**The Chairman**
**APHFTA Lake Zone**
**Ghana Green view along airport road.**
**P. O. Box 2932**
**MWANZA**
**E-mail: dr_ndauzi@live.com**

**Only shortlisted candidates will be contacted.**

216376602

## Fisi alivyoua mtoto, kuzikwepa risasi 49

**Na Halima Ikunji,** KALIUA

MNYAMA fisi amevamia nyumba na kunyakua mtoto Mazoya Nghanya (1) akiwa kitandani na kukimbia naye kabla ya kumjeruhi na kusababisha kifo.

Kadhalika, watu watatu wamejeruhiwa na moja amelazwa katika hospitali ya rufani ya Mkoa wa Tabora ya Kitete.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Safia Jongo, alisema tukio hilo lilitokea juzi saa 9 usiku katika Kijiji cha Kangeme Kata ya Zungimlole Wilaya ya Kaliua mkoani Tabora.

Alisema I katika Hifadhi ya Luganzo fisi huyo alitoka hifadhini na kuingia ndani ya nyumba ya Nhganya Mayala (45) na kumchukua kitandani mtoto Mazoya Nhganya na kukimbia naye. Kamanda huyo alisema askari wake walipambana na kufanikiwa kumuua fisi, lakini katika mapambano hayo risasi 49 zilipotea kutokana na kuzikwepa kabla ya kumuua.

Aidha, alisema katika tukio hilo watu watatu akiwamo baba mzazi wa mtoto hiyo walijeruhiwa, walipojaribu kumshambulia fisi huyo. "Baadhi ya wananchi waliposikia lile tukio na katika kupambana na yule fisi, aliwajeruhi watu watatu na mmoja yupo Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Tabora ya Kitete, na hali yake ni mbaya,'' alisema.

Aliongeza kuwa polisi wakishirikiana na maofisa wanyamapori walikwenda kukagua tukio hilo kuona hali ilivyo fisi huyo aliibuka tena na kuanza kuwashambulia askari na watu waliokuwa wakitoa taarifa kwa askari.

Baadhi wa wananchi wa Kijiji cha Kangeme walisema kuna fisi wengi katika eneo la hifadhi hiyo.

Kamanda aliwataja watu waliojeruhiwa ni baba wa mtoto huyo, Nganya Mayala 45, ambaye aling'atwa kigaja cha mkono wa kulia, Ngezi Lega aliyeng'atwa mkono wa kushoto na paja na Tule Malongo, aliyevunjwa taya na kung'atwa mkono wa kushoto.

# W'biashara sasa kupata mkopo CRDB wa kutoa mizigo bandarini

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya CRDB imesaini mkataba wa makubaliano na Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania (JWT) kuwezesha kulipia gharama za kutoa mzigo bandarini.

Akizungumza katika hafla hiyo ya utiaji saini, Ofisa Mkuu wa Biashara wa CRDB, Dk. Joseph Witts, alisema ushirikiano huo utawawezesha wafanyabiashara kulipia gharama za kutoa mizigo bandarini kwa mkopo (Post Import Financing Solution) na kuondokana na changamoto za ucheleweshaji wa mizigo ambazo huongeza gharama.

Dk. Witts alisema huduma hiyo ni sehemu ya jitihada zinazofanywa na Benki ya CRDB kuunga mkono jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita katika kuboresha mazingira ya biashara kwa wafanyabiashara nchini.

Alisema ili kutoa unafuu zaidi kwa wafanyabiashara, benki hiyo imepunguza riba katika huduma hiyo na wateja watakuwa wakitozwa asilimia 16 kulinganisha na asilimia 18 inayotozwa katika mikopo ya kawaida.

Katika makubaliano hayo CRDB itakuwa ikisaidia kulipa gharama za kutoa mizigo bandarini na wafanyabiashara kulipa katika kipindi cha miezi mitatu.

Akielezea taratibu za upatikanaji wa huduma hiyo, Dk. Witts alisema huduma hiyo itatolewa kwa wafanyabiashara ambao ni wanachama wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania.

"Mkopo huu hutolewa kulingana na kiwango cha gharama za malipo ya mzigo uliopo bandarini ambapo mfanyabiashara anaweza kulipia gharama za kodi ya forodha, gharama za bandari na wakala wa meli kwa wakati na bila kuchelewa," aliongezea Dk. Witts na kufafanua kuwa riba hiyo inaweza kupungua zaidi kutokana na mwitikio na uaminifu utakao kuwa ukionyeshwa na wafanyabiashara.

Mkopo huo wa gharama za tozo/ kodi ya mizigo iliyoagizwa kutoka nje inatolewa kwa masharti nafuu bila ulazima wa kuwa na dhamana ya mali isiyohamishika na hutolewa kwa riba nafuu na mteja atapata fedha kwa muda mfupi usiozidi siku saba atakapowasilisha ombi la mkopo.

Aidha, malipo ya kodi na gharama za kodi na bandari zitalipwa moja kwa moja kwenye taasisi husika ikiwamo TRA, TPA au Wakala wa meli. Dk. Witts alisema wamefanya hivyo ili kusaidia na kurahisisha ulipaji kodi kwa wakati. "Dhumuni letu ni kuleta urahisi kwa wafanyabiashara kupata bidhaa/ mizigo yao pindi wanapoagiza kutoka nje. Vilevile huduma hii itasaidia jitihada za serikali kukusanya kodi kwa wakati na kuboresha uchumi wa nchi kwa kuhakikisha wafanyabiashara wote wanalipa kodi katika muda uliowekwa kama ambavyo serikali imekua ikisisitiza," alisema Dk. Witts.

Alisema huduma hiyo itatoa nafuu kwa wafanyabiashara kipindi hiki cha corona wakati biashara nyingi zimepata changamoto.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Nchini, Mchungaji Silva Kiondo aliishukuru Benki ya CRDB kwa kutambua umuhimu wa wafanyabiashara kupitia jumuiya hiyo na kubuni huduma hiyo ambayo itakwenda kuondoa changamoto nyingi wakati wa uingizaji wa bidhaa nchini.

"Tunajivunia kwa Jumuiya yetu kufikia mafanikio haya, malengo yetu ni kuona wanachama wetu wanafanya biashara zao bila usumbufu wa aina yoyote. Nitoe wito sasa kwa wafanyabiashara wanaoagiza bidhaa nje kutumia fursa hii kuboresha biashara zao," alisema Mchungaji Kiondo huku akisema jumuiya hiyo imejipanga kukamilisha na kuhakikisha inawahudumia kikamilifu wafanyabiashara ili wawe na uhakika na biashara zao.




Ofisa Mkuu wa Biashara wa Benki ya CRDB, Dk. Joseph Witts (wa pili kushoto), akibadilishana mkataba na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara nchini (JWT), Mchungaji Silva Kiondo, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kutiliana saini mkataba wa makubaliano utakaowawezesha wafanyabiashara kupata mkopo wa kulipa gharama za kutoa mizigo bandarini kwa riba nafuu. Wengine ni Mkuu wa Kitengo cha Biashara cha Benki hiyo, Toyi Ruvumbangu (kushoto) na Mkurugenzi wa Mawasiliano JWT, Stephen Chamle. PICHA: **MPIGAPICHA WETU**

# Wanafunzi 100 ufamasia kupata ufadhili India

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO Kikuu cha CT kilichoko katika mji wa Punjab nchini India, kimetoa ufadhili wa nusu ada kwa wanafunzi 100 Watanzania wanaotaka kusomea ufamasia kwenye chuo hicho.

Ofa hiyo ilitangazwa jana na Mkurugenzi wa Idara ya Kimataifa ya chuo hicho, Sourabh Chaudhary.

Alikuwa akizungumza na wanafunzi na watu mbalimbali wanaotembelea maonyesho ya vyuo vikuu yanayoendelea kwenye viwanja vya Mnazimmoja jijini Dar es Salaam.

Chuo hicho na vingine tisa vimekuja nchini kuonyesha kozi wanazotoa kwenye maonyesho hayo kwa mwamvuli wa wakala mkubwa wa elimu nje ya nchi, Global Education Link (GEL).

Alisema wanafunzi wote 100 watakaopenda kusoma fani hiyo kwenye chuo hicho watapata punguzo maalum (Scholarship) hadi asilimia 50 na utaratibu wa safari utakuwa mwezi Agosti.

Alisema kwa wanafunzi ambao bado wako kwenye mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT) wao wataingia chuoni kuanzia mwezi Septemba.

Sourabh alisema urafiki kati ya Tanzania na India ni wa miaka mingi na Serikali ya Tanzania imewekeza kwa kiasi kikubwa katika sekta ya afya ni dhahiri inahitaji wataalamu wa kutosha kuhudumia sekta hiyo.

Alisema pia Serikali ya Tanzania imejitahidi kuboresha miundombinu kwa wanafunzi wa sayansi wakiwapo wanaotaka kusoma kozi za afya. "Kwa kutumia urafiki baina ya nchi hizi mbili uongozi wa chuo umekubaliana ni vyema kuchagua kozi ambayo ina umuhimu na uhitaji mkubwa katika soko la ajira kwa kuipunguzia gharama ili Watanzania wengi waweze kuisoma kwa maendeleo ya nchi na taifa kwa ujumla," alisema.

Aliwahakikishia wazazi kwamba wanafunzi kutoka Tanzania huwa wanafanya vizuri kutokana na maandalizi mazuri katika elimu ya sekondari na wengi wao hupokea tuzo mbalimbali kutokana na umahiri wao wa kufanya vizuri, kujishirikisha na michezo na kuonyesha tabia njema wawapo chuoni.

Alisema mbali na kozi hiyo ya famasia zipo kozi nyingi akitaja baadhi kuwa ni uhandisi, sanaa na paramedics na artificial intelligence kwa uchache.

## Maelfu wanufaishwa mafunzo stadi za kilimo

**Na Elizabeth Zaya**

WAKULIMA 2,176 wakiwamo wanawake 1,294 na wanaume 882 wa mikoa ya Morogoro, Iringa na Njombe wamenufaika na mafunzo ya stadi katika kilimo na ufugaji yaliyotolewa kupitia mradi wa Tajirika na Kilimo unaotekelezwa na Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA), Shirika la Kimataifa la CARE na Taasisi ya Ukuzaji Kilimo Uwanda wa Kusini mwa Tanzania (SAGCOT).

Akizungumza wakati wa kikao cha tathmini ya utekelezaji wa mradi huo, Mratibu wa mradi huo kutoka VETA, Perecy Ugula, alisema wakulima hao walipatiwa mafunzo ya ufugaji bora wa mifugo hususani ng'ombe wa maziwa na kuku, kilimo cha mazao mchanganyiko, na cha mboga na matunda.

Ofisa Tathmini na Ufuatiliaji wa Shirika la Kimataifa la CARE, Edwin Sallu, alisema kupitia utekelezaji wa mradi huo, wamegundua uwapo wa uhitaji mkubwa wa mafunzo stadi za kuboresha shughuli za kilimo kwa wakulima wadogo vijijini.

Sallu alisema mafunzo hayo yamesaidia kuunda vikundi 141 vya uzalishaji katika sekta ya kilimo cha mazao mchanganyiko, mboga na matunda na ufugaji wa kibiashara na kwamba kwa sasa wanafanya shughuli zao za kilimo kwa umoja, hali inayowezesha uzalishaji mazao kwa wingi, ubora na uhakika wa kufikia masoko ya bidhaa zao pamoja na kukopesheka kwa urahisi na kupata faida.

"Kwa kweli tumeshuhudia manufaa makubwa ya mafunzo yaliyotolewa kupitia mradi huu kwa wakulima vijijini, hasa ukizingatia kuwa asilimia 67 ya wanufaika ni wanawake na watoto wa kike ambao tunaamini wataleta mabadiliko chanya kwenye jamii zao," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Ugani kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Kejeri Gillah, alishauri kuweka mkakati wa uendelezaji wa shughuli zilizofanywa kwenye mradi huo ili wakulima wengi zaidi wanufaike na mafunzo hayo.

Mkurugenzi wa VETA Kanda ya Nyanda za Juu, Susan Magani, alisema mamlaka hiyo inaendelea na jitihada mbalimbali za kuhakikisha mafunzo ya ufundi stadi yanawafikia wananchi wengi zaidi hasa maeneo ya vijijini na kwamba anaamini kuwa wakulima wengi zaidi nchini watanufaika na mafunzo hayo ili kuboresha shughuli zao.

Mradi wa Tajirika na Kilimo ulianza kutekelezwa mwaka 2018 kwa lengo la kujenga na kuimarisha ujuzi katika sekta ya kilimo kwa wakulima 2,200 na unatarajiwa kumalizika Desemba mwaka huu.

# Wananchi wamilikishwa viwanja zaidi 500 kusini

**Na Munir Shemweta,** MTWARA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amesema wizara yake imepima viwanja 594 katika eneo linalozunguka Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kusini na kumilikishwa kwa wananchi.

Akizungumza wakati wa uwekaji jiwe la msingi katika hospitali hiyo uliofanywa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Philip Mpango, jana, Dk. Mabula alisema, pamoja na ujenzi wa hospitali hiyo kwa ajili ya kutoa huduma za kitabibu, Wizara ya Ardhi iliona umuhimu wa kupima viwanja eneo hilo na kumilikisha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi na shughuli nyingine.

"Pamoja na ujenzi wa hospitali hii uliofanywa na Shirika letu la Nyumba la Taifa, wizara imepima na kumilikisha jumla ya viwanja 594 kuzunguka hospitali hii ili kuwezesha wananchi kujenga nyumba za makazi na shughuli nyingine," alisema Dk. Mabula.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, NHC imekuwa ikifanya kazi nzuri katika miradi mbalimbali na ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Kusini itakayohudumia mikoa ya Mtwara, Ruvuma na Lindi ni moja ya miradi mikubwa ya kimkakati iliyotekelezwa na shirika hilo.

Dk. Mabula alisema mradi mwingine wa kimkakati unaojengwa na NHC ni wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mara iliyopo eneo la Kwangwa na miradi ya ujenzi wa nyumba na ofisi za Wakala wa Huduma za Misitu (TFS). Alimwomba Makamu wa Rais kulisaidia Shirika kupatiwa miradi ya ujenzi na Taasisi za Serikali kwa kuwa shirika hilo kwa sasa liko imara na lina uwezo wa kujenga miradi ya ujenzi iliyo na ubora wa hali ya juu.

Kwa upande wake Makamu wa Rais, Dk. Mpango alilipongeza Shirika la Nyumba la Taifa kwa ujenzi wa jengo hilo alilolieleza kuwa lina ubora usio na mashaka.

Alizitaka taasisi za serikali zenye miradi ya ujenzi kutoa kipaumbele kwa NHC katika ujenzi wa miradi yake na kulitaka Shirika la Nyumba la Taifa kuzingatia ubora wakati wa utekelezaji miradi na kuhakikisha miradi inakamilika kwa wakati na vifaa vya ujenzi kwenye miradi hiyo vinatoka nchini Tanzania.

Alilitaka shirika hilo kukamilisha ujenzi wa mradi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kusini kwa wakati kama lilivyoahidi na kusisitiza kuwa, ujenzi wa hospitali hiyo ukamilike kwa wakati na kufikia Oktoba, mwaka huu wananchi waanze kupata huduma.



Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Lindi, Tecla Ungele (kulia), akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Anna Magoha, wilayani Liwale juzi, alipotembelea shuleni hapo kusikiliza changamoto mbalimbali zinazowakabili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sababu kushindwa kupunguza vifo vya uzazi zaelezwa

**Na Pendo Thomas,** KIGOMA

WANAWAKE wenye kiwango kidogo cha elimu na ambao hawakwenda shule kabisa wametajwa kushindwa kujisimamia dhidi ya mfumo dume katika kupanga na kuamua idadi ya watoto wa kuzaa hali inayorudisha nyuma jitihada za serikali za kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi.

Akielezea vikwazo mbalimbali walivyobaini katika utendaji kazi wao, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Kasulu, Robert Rwebangira, amesema licha ya elimu wanayoitoa kila siku kwa wanawake kuhusu afya ya uzazi, bado jitihada hizo hukwamishwa kutokana na wanawake kuathiriwa na mfumo dume katika kufanya uamuzi.

Alisema wamebaini wanawake waliopata nafasi ya kufika kidato cha nne na kuendelea wanasimamia maelekezo ya wataalamu wa afya hata inapotokea wamepishana mitazamo na wenza wao.

Rwebangira alisema kitaalamu inapaswa mtoto azaliwe wakati aliyemtangulia akiwa na umri wa miaka mitatu ili kutoa nafasi kwa afya ya mama na mtoto ikiwamo mtoto kunyonya kwa miaka miwili jambo ambalo utekelezaji wake kwenye jamii ni hafifu.

Alisema mwanamke kushindwa kupishanisha watoto inasababisha kuzaliwa wakiwa na kilo chini ya kilo 2.5 au chini ya hizo, hali ambayo pia husababisha watoto wengi wa aina hiyo kupoteza maisha kutokana na kuhitaji uangalizi mkubwa kutoka sehemu za kutolea huduma za afya.

Alitaja tofauti na vifo kuna madhara ya ulemavu wa akili kwa watoto, utapiamlo na udumavu unaosababishwa na mtoto kutokunyonya ipasavyo pamoja na mama kushindwa kumudu kuhudumia vizuri watoto hao kwa wakati mmoja ikiwamo uandaaji wa chakula kulingana na umri wao.

Katika kutafuta uelewa wa jamii hasa kutoka kwa kundi la wanawake ambao hawakupata elimu, Nipashe iliongea na mama mmoja mkoani hapa kwa sharti la kutokutajwa jina, ambaye kwa sasa ana watoto tisa na upishanishaji wake si kama wataalamu wanavyoagiza, kuwa mtazamo wake katika masuala ya uzazi ni kuwa anasikiliza mume wake atakavyoamua japo idadi hiyo kubwa imeanza kumpa hofu.

"Napaswa kumsikiliza mume wangu anavyohitaji, lakini kwa ninavyoona kupata mtoto mwingine baada ya huyu wa tisa inaweza hatarisha maisha yangu," alisema.

# Mpango wa HakiElimu ulivyosukwa kuinua elimu

**Na Elizabeth Zaya**

TAASISI ya HakiElimu imezindua mpango kazi wake wa miaka mitano unaotarajia kuanza mwaka kesho hadi mwaka 2026.

Akizungumza katika hafla ya kumbukumbu ya miaka 20 tangu kuanzishwa kwa taasisi hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa HakiElimu, Dk. John Kalaghe, alisema katika mpango huo wa miaka mitano yapo mambo mengi ambayo watayafanyia kazi likiwamo eneo la lugha, usawa wa kijinsia kwenye sekta ya elimu, elimu jumuishi hususani kwa watoto wenye ulemavu.

Nyingine alisema ni elimu ya awali, ulinzi wa watoto shuleni na nje ya shule, teknolojia na ubunifu kwenye sekta ya elimu, pamoja na kuingiza masuala ya mabadiliko ya tabia nchi kwenye elimu. Dk. Kalaghe alisema yapo mambo mengi yamefanywa katika kipindi hicho ambayo yalichangiwa na ushirikiano wa wadau mbalimbali kwenye sekta hiyo.

"HakiElimu katika miaka hii 20 tangu kuanzishwa kwake, imefanya mambo mengi, lakini yote hayo yametokana na mchango mkubwa kutoka kwa wadau mbalimbali," alisema Dk. Kalaghe.

"Safari yetu ilikuwa na mambo mengi na tusingeweza kufika hapa bila ushirikiano wa serikali, wadau mbalimbali wa elimu ambao wamekuwa nguzo kubwa ya haya yote," alisema Dk. Kalaghe.

Dk. Kalaghe alisema katika kukumbuka ya miaka hiyo 20, pia wamezindua kitabu ambacho kitakuwa kinaelezea historia ya taasisi hiyo.

"Kwa miaka hii 20 ya kumbukumbu, HakiElimu imefanya kazi kubwa ya kufanya utafiti unaolenga kuboresha sekta ya elimu nchini na kwa asilimia kubwa imefanikiwa japokuwa bado tunatakiwa kuendelea kufanya zaidi kwa maboresho zaidi," alisema Dk. Kalage. Kwa upande wake, Balozi wa Uswisi nchini, Anders Sjoberg, alisema elimu ni miongoni mwa haki za msingi hivyo inatakiwa ipatikane kwa kila mtu bila kujali hali yake.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, alisema baadhi ya maeneo ambayo HakiElimu imepanga kuyafanyia kazi katika mpango kazi wake wa mwaka 2022/26 itasaidia sana kuboresha sekta hiyo kwa sababu tayari serikali nayo imeyawekea mpango wa kuyaboresha.

"Tunaipongeza HakiElimu kwa jitihada zake ambayo imekua ikizifanya katika sekta hii, kama serikali tumekuwa tukifanya nao kazi pamoja japokuwa kila mmoja anakwenda kwa approach yake," alisema Prof. Nombo.



Wanaumoja wa Taasisi ya Tanzania Peace (TPF), wakifanya usafi katika Hospitali ya Mwananyamala, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, baada ya kukabidhi misaada ya vitu mbalimbali hospitalini hapo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Sekta binafsi yapumua uchangiaji WCF

**Na Mary Geofrey**

MFUKO wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), umepunguza kiwango cha mchango wa wafanyakazi wa sekta binafsi kutoka asilimia 1.0 hadi asilimia 0.6 ya mapato ya waajiriwa.

Mabadiliko hayo ni kwa mujibu wa tangazo la serikali namba 496G la Juni 30 mwaka huu kufuatia bajeti ya serikali ya mwaka wa fedha 2021/22 iliyopitishwa na bunge kupunguza tozo mbalimbali.

Mkurugenzi Mkuu wa WCF, Dk. John Mduma, akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam, alisema punguzo hilo la tozo ni sawa na asilimia 40 ya makato aliyokuwa anawasilisha mwajiri kwa ajili ya mwajiriwa. Kadhalika, alisema sekta ya umma walikuwa wakichangia asilimia 0.5, ya mapato ya wafanyakazi na kwamba utaendelea kubaki kama ulivyo.

Alisema licha ya kupunguzwa kwa tozo hizo zinazomnufaisha mwajiri na mwajiriwa, hazitaathiri mafao ya fidia kwa wafanyakazi ambao wataumia, kuugua au kufariki kutokana na kazi wanazofanya kwa mujibu wa mikataba ya ajira zao.

Alisisitiza kuwa, kupungua kwa kiwango hicho hakutaathiri mfuko kwa sababu una uwezo wa kujiendesha kwa zaidi ya miaka 30 na kwamba kupitia punguzo hilo wanatarajia kupata wanachama wengi zaidi.

"Kiwango hiki kipya kitapunguza gharama za uendeshaji kwa waajiri wa sekta binafsi, kuboresha mazingira ya kufanya biashara za uwekezaji nchini na kuboresha na kuimarisha uhusiano mzuri baina na waajiri na WCF," alisema Dk. Mduma. Aidha, alisema kutaongeza utekelezaji kwa waajiri kujiunga katika hifadhi ya jamii kwa sababu punguzo litawasaidia waajiri kuboresha mikataba yao na waajiriwa.

"Pamoja na kushuka kwa tozo za uchangiaji katika Mfuko kwa waajiri, mafao ya fidia yataendelea kulipwa kama ilivyokuwa na kwa mujibu wa Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi na Kanuni zake za mwaka 2016," alisema Dk. Mduma.

# Vyuo vikuu 10 vya nje kusaka wabia nchini

**Na Joseph Mwendapole**

VYUO vikuu 10 kutoka nje ya nchi viko nchini kwa ajili ya kuelezea fani wanazofundisha na kutafuta ubia na vyuo vya nchini katika utoaji wa elimu ya fani mbalimbali.

Vyuo hivyo nane kutoka nchini India na viwili kutoka Ukraine vimekuja kwa mwamvuli wa wakala wa vyuo vikuu nje ya nchi Global Education Link (GEL), kwa ajili ya kushiriki maonyesho ya vyuo vikuu yaliyoandaliwa na Tume ya Vyuo Vikuu (TCU).

Maonyesho hayo ya siku tano yanayoshirikisha vyuo vikuu na taasisi mbalimbali yalianza Jumatatu jijini Dar es Salaam.

Mkurugenzi wa GEL, Abdulmalik Mollel alivitaja vyuo hivyo ni Chandigarh, Lovely Professional University (LPU), CT, Maharish Makandeshwar, Pandeet Deendayal Energy, Sharda, Rayat Bahra vya India na VN Karazan na Sum State vya Ukraine.

Alisema baadhi ya vyuo vimeahidi kufungua matawi nchini baada ya kuona mahitaji makubwa ya kozi wanazofundisha ambazo wanafunzi wa Tanzania wamekuwa wakizifuata kwenye mataifa yao.

Alisema pia baadhi ya vyuo hivyo vya nje vitaingia makubaliano na vyuo vya nchini kuhusu namna ya kufanyakazi pamoja katika utoaji wa elimu ya juu.

Mollel alisema ujio wa vyuo hivyo ni fursa kwa vyuo vya Tanzania kuangalia namna ya kushirikiana kwenye kozi mbalimbali ikiwamo kubadilishana wanafunzi wanaoendelea na masomo ili kupeana uzoefu.

# TFS: Jivunieni chanzo cha maji Mto Ruvuma

**Na Elizabeth Zaya**

KAMISHNA wa Uhifadhi wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Prof. Dos Santos Silayo, amewataka wakazi wa mkoa wa Ruvuma kujivunia na kuhifadhi chanzo cha maji cha Mto Ruvuma kilichopo katika milima ya Matogoro Manispaa ya Songea.

Prof. Silayo alisema hayo mkoani Ruvuma alipoongoza msafara wa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, kupanda msitu wa milima ya Matogoro kwa ajili ya kujionea mapango na chanzo cha maji cha Mto Ruvuma ikiwa ni sehemu ya maazimisho ya Tamasha la Majimaji Selebuka linalofanyika wilayani Songea.

"Mto Ruvuma umeubeba Mkoa wa Ruvuma kwa kuwa umepita katika wilaya zote tano ...na ni kwa sababu hii wananchi kwa kushirikiana nasi TFS tunapaswa kuuheshimu na kuulinda msitu huu," alisema Prof. Silayo.

Mhifadhi Mkuu Kanda ya Kusini, Manyisye Mpokigwa, alisema chanzo cha Mto Ruvuma licha ya kuwa ni muhimu kwa wakazi wa mkoa huo, pia ni kivutio cha utalii.

Alisema kisima hicho ndicho kinaunda Mto Ruvuma ukiwa na urefu wa kilomita zaidi ya 800, upana wa kati ya mita 300 hadi 500 kutegemea na eneo lililopo.

## Anna Mghwira

Mgombea urais mwanamama wa kwanza kutambuliwa, kuenziwa

Ukurasa 12





Ukurasa 14

## DK. OMAR ALI JUMA Mwasisi mkakati Tanzania kuufikia uchumi wa kati


# siasa

JUMATANO JULAI 28, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe


TOZOUMIZA MUAMALA

# Wabunge wavae uhusika unaotetea wapigakura wao

Na Christina Mwakangale

MFUMO mpya wa tozo za miamala ya simu ulioanza kutozwa Julai 15, mwaka huu, ni matokeo ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2021/22 iliyopitishwa na wabunge kwenye bunge la bajeti mjini Dodoma mwezi uliopita.

Mabadiliko ya kisheria ya aina yoyote huanzia bungeni huku wawakilishi wakiwa tegemeo la wapigakura kuwa kile wanachokipitisha kinakuwa na tija na kulinda maslahi ya wananchi walio katika makundi na viwango mbalimbali.

Bunge limepitisha tozo hizo ambazo hadi kuwa sheria na kuanza kutumika zimelalamikiwa kupindukia na swali la kuwauliza wabunge hao linabakia kuwa walivaa uhusika wa mwananchi wa kawaida, hususan aliyepo kijijini wakati wanapitisha sheria hiyo? Au walitazama nini kwa vile tegemeo kubwa la Watanzania hao ni kupata huduma za kifedha kupitia simu za mkononi.


TISHIO KIBIASHARA

Tozo hizo 'umiza' , tayari zimetua kwenye Chama cha Waendesha Huduma ya Simu za Mkononi Tanzania (TAMNOA), wakitoa tathmini inayoonyesha kuwa huenda zikawa kitanzi kwa biashara za fedha kupitia simu za mkononi.

TAMNOA, imeanza wiki kwa kutoa tathmini ya athari zilizotokana na tozo za miamala kupanda, ikisema wateja zaidi ya 1,000,000 hususani walioko vijijini walisitisha kutumia huduma na kwamba miamala imepungua kwa asilimia 45.

Mwenyekiti wa TAMNOA, Hisham Hendi, ambaye pia ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa VODACOM, anasema kwamba Sheria ya Fedha ya mwaka 2021/22, iliyopitishwa bungeni ni namna mpya ya utozaji kodi katika kila muamala unaofanywa na mteja kwa njia ya simu za mkononi.

Hendi, anasema wateja walioko vijijini wamesitisha kutumia huduma za miamala ya simu, kutokana na ongezeko la makato, ambayo aliyataja kama tishio kwenye uhai wa biashara ya simu nchini.



Waziri wa Fedha, Mwigulu Nchemba na mkoba wa bajeti ya serikali ya 2021/22 iliyoanzisha tozo mpya ya miamala iliyoanza kutumiwa mwezi huu. **PICHA MTANDAO.**

Huduma za kifedha kwenye simu za mkononi, kutuma na kupokea zinakua, kwa mujibu wa Waziri wa Mawasiliano ya Teknolojia ya Habari Dk. Faustine Ndugulile, hadi Desemba mwaka jana kadi za simu milioni 51 zilikuwa zimesajiliwa na asilimia 48.6 kati ya hizo, inafanya miamala mbalimbali.

Ripoti ya hali ya uchumi Tanzania ya Juni 2020 iliyotolewa na Benki ya Dunia (WB), inaonyesha asilimia 23.4 pekee ya wakazi wa mijini wana akaunti benki na asilimia 5.1 ya wanaoishi vijijini wana akaunti za benki, hivyo Watanzania wengi hujumuishwa kwenye huduma za kifedha kupitia simu za mkononi.

Kupanda kwa tozo katika kila muamala unaofanywa na wateja wa kampuni mbalimbali za simu, kumeibua mjadala miongoni mwa wananchi, huku wataalamu wa uchumi na viongozi wakilitolea suala hilo ufafanuzi na kuahidi kulifanyia kazi upya suala hilo.

Tozo hizo zinamtoza kila anayefanya muamala wa Sh. 100,000 zaidi ya Shilingi 6,000 kiwango hicho kinazidi kupanda kadri muamala wa fedha unavyoongezeka.

Kwa wananchi wa hali ya chini ambao hufanya miamala kila siku iwe kutuma au kupokea fedha na kulipia huduma za kijamii, wapo wanaofanya muamala mdogo kwa usiozidi Sh. 5,000 kwa mawakala, ili atekeleze majukumu yake, wote hao wameathirika na wameumia.

Mtaalamu wa masuala ya fedha kutoka Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) cha Dar es Salaam, Profesa Bill Kiwia, anadokeza kuwa ongezeko hilo la kodi ya tozo, litaleta athari za moja kwa moja kwa wananchi.

Waziri wa Fedha na Mipango Dk. Mwigulu Nchemba, akiwasilisha bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha wa 2021/2022 anasema jumla ya bajeti iliyotengwa ni Sh. trilioni 36.33, matumizi ya kawaida yatakuwa Sh. trilioni 23 huku ya maendeleo ikiwa Sh. trilioni 13.3.

Bajeti hiyo imepandisha takribani mara mbili gharama za muamala zilizokuwa zinatozwa awali hali inayolalamikiwa na sasa Dk. Nchemba, anaahidi tozo hizo zitaangaliwa ila amefafanua kuwa uwepo wake ni sheria ya bunge, ambayo yeye hawezi kuifuta na kitakachofanyika ni kupitia kwa kanuni na kuangalia utekelezaji wake.

Aidha, pendekezo la kutoza Sh. 10 hadi 200 kwa kila laini ya simu kulingana na uwezo wa kuongeza salio, ni mwiba na suala jingine ambalo linaigusa jamii.

**MAMBO YA KUANGALIA**

Wakati Waziri Nchemba anaongeza tozo za miamala ya simu , bunge hilo limetoa msamaha wa kodi kwa bia zinazozalishwa na shayiri ya Tanzania kutoka Shilingi 765 kwa lita hadi 620 kwa kipimo hicho.

Lakini, pia Waziri analitangazia bunge kupunguza kodi ya mabasi yanayoagizwa nje ya aina ya mwendokasi, kadhalika viwanda vya sabuni navyo vimepunguziwa kodi na michezo ya kubashiri au kamari zimepunguziwa kodi kutoka asilimia 25 mpaka 15

Aidha, simu za janja aina ya vishikwambi , vimeondolewa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na pia vifungashio vya tumbaku vimefutiwa ushuru ili kuhamasisha viwanda vya kuchakata na kuzalisha sigara kwa wingi nchini.

Pengine katika orodha ya vitu vilivyopewa punguzo la kodi vingi vinahusisha masuala ya starehe kama pombe, sigara michezo ya kubashiri kununua simu janja za vishikwambi (ipad) na huenda ingefaa kodi zake ziwe juu zaidi badala ya msamaha.

Watanzania wanasubiri jopo la watalaamu wanaoangalia tozo za miamala kutoka Benki Kuu (BoT), Mamlaka ya Mwasiliano (TCRA), Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, kuja na maelezo yatakayowaongezea amani badala ya machungu.

Serikali inashauriwa kuzifikia kampuni kubwa kama Netflix na Youtube zinatengeneza faida kwa kutoa huduma zao hapa nchini na wachumi wanashauri serikali kuzitoza kodi kampuni hizo na kwamba Kenya tayari inafanya hivyo.

# Kambaya anavyowasikitikia vijana, ataka waandaliwe kutwaa uongozi



Abdul Kambaya, Mjumbe wa Baraza Kuu la Uongozi CUF Taifa. **PICHA: MAKTABA**

**Na Sabato Kasika**

VIJANA ni taifa la leo na wanatakiwa kujengwa katika misingi ambayo itawafanya wawe viongozi wa baadaye, lakini pia wawe wazee wenye busara na hekima ambao ni hazina kwa vizazi vijavyo.

Ushiriki na mchango wao unahitajika katika uhai wa taifa, na kwamba kinyume cha hapo, nchi inaweza kukosa viongozi makini wa baadaye kadhalika kuwa na wazee wasio na manufaa kwa jamii zao, anasema Abdul Kambaya, Mjumbe wa Baraza Kuu la Uongozi la CUF Taifa.

Anasema ni kutokana na umuhimu huo, serikali inapaswa kuandaa mazingira rafiki kwa vijana ili waweze kushiriki katika masuala ya kisiasa, kwa kuwa hiyo ni miongoni mwa mambo yanayofanikisha kupata viongozi bora wa baadaye.

Kambaya anasema hayo katika mazungumzo na gazeti hili jijini Dar es Salaam na kudai kuwa vijana nchini hawawekewi mazingira ya kuandaliwa kuwa viongozi wa taifa kwa siku sijazo.

"Lakini kwanza nifafanue kuwa, vijana wanapoandaliwa kuwa viongozi, si lazima wawe wanasiasa, bali wanaweza kuongoza taasisi za umma za binafsi na hata za kijamii na kufanikisha kufikiwa makusudi na malengo tarajiwa," anasema Kambaya.

Anaongeza kuwa vijana wanatakiwa kuchangia maendeleo ya nchi yao, na kwamba hali ilivyo sasa, inaonyesha kuwa huenda wakakosekana viongozi wa baadaye na kupata wazee ambao itakuwa vigumu kuchota busara kwao kama mambo yataachwa kubaki kama yalivyo.

VIJANA MBUMBUMBU

Kambaya anasema, kwa sasa kuna baadhi ya vijana hawajui kinachoendelea katika nchi yao, pia hawatoi maoni na hata linapotokea jambo ambalo wanatakiwa kuchangia mawazo na mikakati hukaa kimya.

"Vijana wengi mijini unawakuta kwenye mitandao ya kijamii, wakiigiza maisha, kuandika mambo ambayo hayana umuhimu na pia wanafuatilia masuala yasiyo na maana kwao wala kwa taifa lao. Lakini idadi kubwa iko vijiweni haina kipato, kazi wala fikra za kimaendeleo," anaonya mjumbe huyo.

> "Mfano, vijana wetu wawe na elimu wasiwe nayo, kupitia miradi mikubwa kama ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) na kufua umeme wa maji kwenye Bwawa la Nyerere inadaiwa kuwa imekuwa na malipo madogo lakini pia inawanufaisha zaidi wageni kuliko Watanzania," anasema.

Anasema, wapo baadhi yao wanaoishi kwa kujipendekeza kwa viongozi, na kwamba wanaona ni jambo la kawaida bila kufanya juhudi zozote za kuwawezesha kuandaliwa kuwa viongozi wa baadaye.

"Ukifuatilia, utagundua kuwa, kwa sasa wapo baadhi ya vijana hawajui hata kuhusu corona, hawana taarifa za chanjo yake, hawafahamu kuwa Tanzania imeagiza chanjo tena hawana habari ya katiba inayowaongoza wala mahitaji ya katiba mpya," anasema Kambaya.

Anaonya kuwa nchi ikishakuwa na vijana ambao hawajui hayo na badala yake wanaishia kusoma magazeti ya udaku, mambo ya mitandao yasiyokuwa na tija, kukimbia kazi, masomo na kuishi vijiweni huku wakipuuza mambo ya msingi, miaka ijayo nchi inaweza kuingia gizani.

"Kiongozi wa nchi husaidiwa kiuchumi, kifikra na vijana, hivyo wanatakiwa kuandaliwa vyema ili waondokane na mambo yasiyokuwa na tija na serikali iwajibike kuhakikisha vijana wanakuwa sehemu ya maendeleo ya nchi hii,"

**HATUA ZA KUCHUKUA**

Mjumbe huyo anasema, si katika siasa tu, bali serikali inatakiwa kuwafanya vijana kuwa sehemu ya maendeleo ya uwekezaji, biashara na uchumi, badala ya kubaki watazamaji na ni vyema iwekeze kuanzia kwenye elimu na afya kwa vijana ili kulinda au kuwa na mtaji wa watu wenye siha na weledi kuliko ilivyo sasa.

Anasema, moja ya changamoto iliyopo kwenye elimu kwa mtazamo wake ni mitaala na madaraja kushindwa kumuandaa kijana kuwa na ujuzi wa kuajiriwa au kujiajiri kwa vile muda wote huwa darasani na kila anapofaulu kwenye daraja unakuwa msingi wa kwenda kwenye jingine.

Mfano, akitoka shule ya awali anakwenda shule ya msingi, baadaye sekondari na katika vyuo vya ufundi na vikuu lakini viwango vyote hivyo vya elimu, havimpi mwanafunzi ujuzi na maarifa ya kujiajiri zaidi ya kutegemea kuajiriwa, lakini pia haajiriki.

"Ni vyema sasa kwa serikali kuwa na mitaala itakayobaini chaguo na vipaji vya wanafunzi na kisha kuwapa elimu na ujuzi wa kujiajiri kutokana na chaguo lao na vipaji vyao kuliko kuwaacha waendelee kama walivyo," anasema.

**MIFANO YA KUTAZAMA**

Kambaya anatolea mifano ya vipaji vya michezo na sanaa kutoka kwa Mbwana Samatta, Simon Msuva ambao ni wacheza soka wa kimataifa, wanamuziki Diamond na Ali Kiba kuwa kama kungekuwa na mitaala ya kutambua vipaji , soko la uwekezaji na biashara kwa vijana lingekuwa kubwa nchini.

"Lakini kwa vijana waliofanikiwa kupata elimu ya vyuo mbalimbali na hata wale waliokosa elimu, serikali ina mipango gani ili kuhakikisha inawezesha kuingia kwenye soko la uwekezaji na biashara ili wawe sehemu ya maendeleo ya uchumi wa nchi hii? Anahoji Kambaya.

Kambaya anasema, sera zinaweza kuwa nzuri, lakini zikakosa utashi wa kisiasa wa utekelezaji, au zinaweza kuwa si rafiki kwa vijana nchini kwa mukhtadha wa uwekezaji na biashara.

"Mfano, vijana wetu wawe na elimu wasiwe nayo, kupitia miradi mikubwa kama ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) na kufua umeme wa maji kwenye Bwawa la Nyerere inadaiwa kuwa imekuwa na malipo madogo lakini pia inawanufaisha zaidi wageni kuliko Watanzania," anasema.

Anafafanua kuwa Mpango wa Miaka Mitano wa Maendeleo ni vyema utambue umuhimu wa 'mtajiwatu' katika kuutekeleza na kukuza pato la taifa kwa kuwekeza na kutenga fedha kwa ajili ya kuwanyanyua vijana.

Na Ani Jozeni



ANNA MGHWIRA

# Mgombea urais mwanamama wa kwanza kutambuliwa, kuenziwa

KIFO kimeendelea kuwaondoa katikati ya Watanzania viongozi na wana jamii kadhaa na safari hii kimemchukua aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira.

Mama Anna au kama wengi walivyomwita kwa jina la Mama Mghwira, alikuwa mtu wa kipekee nchini kwani ni mwanamke wa pili kugombea urais wa Jamhuri ya Muungano, baada ya wajina wake Anna-Claudia Senkoro kufanya hivyo kwenye uchaguzi mkuu wa 2005.

Anna Senkoro aliyefariki Januari 4, 2017, alikuwa mgombea kutoka Chama cha Progressive Party of Tanzania-Maendeleo (PPT-Maendeleo) na kwa mara ya kwanza aliwatambulisha kinamama kwenye ulingo wa kampeni za kusaka uongozi wa juu kitaifa.

Anna Mghwira naye alijipambanua kwa jitihada hiyo mwaka 2015, akikiwakilisha Chama cha ACT-Wazalendo.

Rais Samia Suluhu Hassan, katika salamu zake kwa wafiwa na taifa anasema mkuu huyo wa mkoa mstaafu alilitumikia taifa kwa uadilifu mkubwa akitaka aenziwe.

Anna Mghwira alikuwa na umri sawa na hayati Dk. John Magufuli, ambaye katika hotuba fupi ya Rais mstaafu Ali Hassan Mwinyi, akizungumza huko Chato kwenye msiba anakumbusha kuwa 'Magufuli bado hajawa au hakuwa mzee.'

Mama Anna alikuwa mwanasiasa ambaye bado anahitajika umri wa miaka 60 kwa wengi ni kiongozi anayechemka anayeweza kuendelea kuongoza Watanzania.

Rais Samia, akizungumza na wazee wa Dar es Salaam takribani miezi miwili, iliyopita anasema umri wa miaka 60 au 61 ni mwanzo wa uzee, naye akajiweka katika kundi hilo.

Ni kweli kama alivyosema Rais Samia kuwa alipokea habari za kifo cha Mama Mghwira kwa masikitiko makubwa kwa sababu ya mchango wake katika uongozi wa taifa, yaani kwa kuibuliwa katika na kuwezesha taifa kwa jumla kupiga hatua mpya kifikra na kimkakati kutokana na uwepo wake.

Inawezekana aliandaliwa kisaikolojia kwa michango yake katika siasa kutokana na kusoma nyanja tofauti za masomo ya ngazi ya juu kwa vile ni mhitimu wa masomo ya Theolojia katika Chuo Kikuu cha Tumaini, tawi la Makumira ambalo kitamaduni ni shule kuu ya theolojia ya Kanisa la Kilutheri.

Halafu akasoma sheria Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, na kupata shahada ya pili ya fani hiyo Chuo Kikuu cha Essex nchini Uingereza mwaka 2000.

Mghwira aliingia katika siasa akitokea katika harakati za mashirika ya kimatifa yenye matawi au miradi hapa nchini na kati ya shughuli hizo kinachotajwa zaidi ni uwezeshaji wa wanawake, maendeleo ya jamii na kuwasaidia wakimbizi, maeneo ambayo yamejikita katika kutoa misaada kwa wanyonge.

Halikuwa jambo la kushangaza kuwa alipoona Rais John Magufuli anasahihisha mielekeo mibovu katika utawala ambao alikuwa anaota kuunyooshea kidole, kwa mfano ule mkakati wa 'kutumbua majipu' hakusita kumuunga mkono.

Waliosema wanaohama kumunga mkono JPM walilipwa, kimsingi hawazifahamu ndoto za washiriki wengi katika siasa au maendeleo ya jamii za kuondoa changamoto katika utawala, kurekebisha pale watu wanapoonewa kwa kudhamiria, watawala wakijikinga kwa sheria.

Kama walivyo wengine waliotoa mchango mkubwa miaka ya karibuni, Anna Mghwira, alihama kutoka upinzani, na kwa upande wake siyo mara moja, kwani mwanzoni alijiunga na CHADEMA mwaka 2009 halafu akajiunga na ACT-Wazalendo mapema mwaka 2015.

Yote hiyo ni kufuatilia hisia kwanza ya kuweza kutoa mchango kutoka upinzani kwani unaweza kujieleza kwa kina au hata kwa hisia kali zaidi, halafu akaona kuna jema lililoibuliwa na wafuasi wa Zitto Kabwe kujitenga.

Ni kati ya hao ambao pia walipatikana waliokiri kuwa JPM alikuwa anafanya kazi adhimu kurekebisha mambo yaliyokuwa yanalalamikiwa serikalini.

Pia kuna vijana kutoka CHADEMA walihama wakati huo, ambao hawakufikia azma kuhama kwenda ACT awali.

Ndiyo hapo hayati Anna Mghwira aliposaidia kubadilisha taswira ya siasa nchini kwani alipata nafasi ya kuwa Mwenyekiti Mwendeshaji wa ACT Wazalendo, nyuma ya kiongozi mkuu ambaye anakuwa kama mdhamini mwandamizi wa chama, ambaye nafasi yake haihitaji kupigiwa kura.

Kwa vile mdhamini na kiongozi mkuu Zitto Kabwe, alikuwa hajafikia tarehe halisi ya umri wa miaka 40 wakati wa kupiga kura 2015 alizuiliwa na sheria kuwa mgombea wa ACT-Wazalendo, hivyo chama kikamteua mwenyekiti mwendeshaji kuwa mgombea.

Hiyo iliwezesha kuwa na nafasi maalum kati ya wale waliohama kumuunga mkono JPM, wengine wakiwa na vyanzo tofauti vya kitaaluma au kiutawala CHADEMA, kuwa tayari ni viongozi wanaokubalika katika jamii, akafanana nao kwa kuteuliwa kugombea.

> Mara alipoingia madarakani Rais Samia alimtambua mwanamama huyo ambaye ni kijana zaidi kwa Mghwira na kwa maana hiyo ameanza harakati za siasa na kufikia utawala serikalini kipindi ambacho kwa umri huo Mghwira alikuwa katika harakati za maendeleo.

Ni baraka ambayo baadaye imemkuta Queen Sendiga, mgombea urais wa ADC- ambayo kama ACT- Wazalendo ila ilitokea CUF, akawa mgombea kutokea nafasi ya Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho.

Mara alipoingia madarakani Rais Samia alimtambua mwanamama huyo ambaye ni kijana zaidi kwa Mghwira na kwa maana hiyo ameanza harakati za siasa na kufikia utawala serikalini kipindi ambacho kwa umri huo Mghwira alikuwa katika harakati za maendeleo.

Ukichukulia kuwa Rais Samia pia alionekana zaidi katika Bunge Maalum la Katiba mwaka 2014 sawa na Naibu Spika Dk. Tulia Ackson na Waziri Ummy Mwalimu unaona kuna kizazi kipya cha viongozi wanawake katika ngazi za juu. Bila shaka Anna Mghwira alitoa mchango adhimu kuyakinisha uwepo wao, uadilifu na udiriki wao.

JUKWAA LA VIONGOZI

DK. OMAR ALI JUMA

# Mwasisi mkakati Tanzania kuufikia uchumi wa kati

## Shujaa kuondoa umaskini, Baba MKUKUTA na NEP



Baadhi ya viongozi wa serikali na jamaa wakiomba dua kwenye kaburi la Dk. Omar lililoko kijijini kwao kisiwani Pemba. **PICHA ZOTE MTANDAO**



Dk. Omar Ali Juma katika harakati za kisiasa.

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

ULIKUWA mwezi Julai mwaka 2001, Watanzania walipotangaziwa kifo cha Makamu wa Rais wa wakati huo, Dk. Omar Ali Juma, haikuwa jambo rahisi kuzikubali taarifa hizo.

Kwa mujibu wa maelezo ya Rais wa awamu ya tatu Benjamin Mkapa, Makamu wake alifariki saa 5:45 usiku wa Jumatano Julai 4 kutokana na matatizo ya moyo.

Hata sasa Watanzania wanamwomboleza kwa kuziangalia kazi zake nyingi alizofanya kwa miaka mitano ya utumishi, kwa ajili ya maendeleo ya taifa na kwa matumaini wanashuhudia masuala muhimu yanayoonekana kuwa na matumaini na mafanikio makubwa leo, ambayo yeye ndiye aliyeanza usimamizi na utekelezaji wake.

Kazi ya kulinda mazingira na kupunguza umaskini ndicho alichokisimamia hata leo Tanzania inatajwa kuwa nchi ya uchumi wa kati, jukumu hilo lilianza na Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Omar.

> Alianza kupunguza umaskini kwa mtu mmoja mmoja hadi taifa lakini heshima yake inabakia kwa mafanikio yanayoonekana kwa mamilioni ya Watanzania ambao wanaendelea kulinda na kuhifadhi mazingira yao na kupunguza umaskini.

Alianza kupunguza umaskini kwa mtu mmoja mmoja hadi taifa lakini heshima yake inabakia kwa mafanikio yanayoonekana kwa mamilioni ya Watanzania ambao wanaendelea kulinda na kuhifadhi mazingira yao na kupunguza umaskini.

Licha ya kuwa Makamu wa Rais alikuwa na tatizo la moyo, kifo chake kilikuja ghafla mno, wakati kiongozi huyo siku ya Julai 3, alionekana kwenye vyombo vya habari akimuaga Rais wa DRC, wakati huo Joseph Kabila.

Mkapa ndiye aliyetangaza kifo chake, akimsifu kuwa alikuwa msaidizi wake mahiri, mwenye sifa za kutukuka, akiwa mwaminifu, mwadilifu na mchapakazi hodari, ambaye aliacha pengo kwenye uongozi wa taifa.

Kwa wengine Makamu wa Rais alionekana kuwa pengine angekuwa mrithi wa Rais Benjamin Mkapa, mwaka 2005 kwenye uchaguzi mkuu.

Dokta Omari Ali Juma, hakuwa mtumishi wa Watanzania peke yao bali pia alikuwa mshiriki mkubwa wa kutafuta amani ya Congo na hata siku alipofariki usiku wa Jumatano Julai 4, jijini Dar es Salaam, mchana huo alikuwa naRais Kabila kufanikisha juhudi za kusaka amani ya Congo.

Mkapa alipotangaza kifo cha Makamu wake, alisema alifariki ghafla saa 5: 45 usiku wa Jumatano. Kiongozi huyo alizaliwa Juni 26,1941.

Kitaaluma alikuwa mtaalamu wa mifugo na mahali anapotokea alikuwa mzaliwa wa kisiwani Pemba na historia yake ya uongozi imeandikwa pia kwenye Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), alipokuwa Waziri Kiongozi.

Waziri Kiongozi Dk. Omar, alifanya kazi hiyo kuanzia Januari 25, 1988 hadi Oktoba 1995 alipoanza rasmi kazi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano.

Mwaka 1988 alikuwa Waziri Kiongozi wakati huo SMZ ilikuwa ikiongozwa na Rais Abdul Idris Wakil na ulipowadia muda wa kuondoka madarakani mwaka 1995 Zanzibar ilikuwa chini ya Salmin Amour Juma.

Dokta Omar pamoja na Mkapa walikuwa wamechaguliwa kuongoza tena Tanzania kwenye uchaguzi wa Oktoba 2000 na alianza kuwa Makamu wake rasmi mwaka 1995.

Jumatano mchana ambayo jioni aliaga dunia, Dk. Omar alikuwa pamoja na Mkapa kwenye mazungumzo ya amani ya Congo yaliyokuwa baina ya viongozi wa Tanzania, Rais wa Uganda Yoweri Museveni na Kabila wa Congo. Katika mkutano huo, Uganda ilidaiwa kuhusika na kuwaunga mkono waasi wa Congo waliokuwa wakipambana na serikali ya DRC.

**TUNU ALIZOACHA**

Dokta Omar anakumbukwa kwa mengi hasa suala la ulinzi, utunzaji wa mazingira pamoja na mikakati ya taifa ya kupunguza umaskini.

Sera ya Taifa ya Mazingira (NEP) iliyoanza kuandaliwa tangu mwaka 1996 na kukamilika mwaka 1997 ni mambo yaliyofanywa chini ya uongozi wa Ofisi ya Makamu ya Rais, Dk. Omar.

Akiwa na jukumu la kufanikisha Mkakati wa Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), Makamu wa Rais, Dk. Omar pamoja na Mkapa, majina yao hayawezi kusahaulika kwenye kuundaa na kutekeleza mpango huo ulioanza mwaka 2001 hadi 2002, kisha 2004 hadi 2005 .

Watanzania watakumbuka kuwa kuanzia katikati ya miaka ya 1990 kipindi ambacho awamu ya tatu iliingia madarakani, suala la kupambana na umaskini lilikuwa ajenda ya dunia na hilo likawa moja ya malengo muhimu ya kuondoa umaskini ili kufikia maendeleo endelevu.

**TANZANIA YA VIWANDA**

Ofisi ya Makamu wa Rais, Dk. Omar ilibeba ajenda ya kuondoa umaskini ambayo kwa Afrika inaanzia kwenye mkutano wa Cairo uliofanyika mwaka 1994.

Baada ya mkutano huo jukumu la kuondoa umaskini lilibebwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, na mikakati mingi kama MKUKUTA ilioandaliwa kuanzia 1997, kisha kufuatiwa na Tanzania Development Vision 2025.

Mpango huo wa muda mrefu ulilenga kuiona Tanzania mwaka 2025 ikiwa ni taifa la uchumi wa kati, taifa la viwanda na lisilo na kiwango kikubwa cha umaskini.

Maono hayo ya Dk. Omar yalitimia mwaka 2020 July, wakati awamu ya tano ilipotangaza kuwa Tanzania imeingia kwenye orodha ya mataifa ya uchumi wa kati.

Japo hakuishi na kuliona taifa likiingia kwenye zama mpya za maendeleo fikra na kazi zake zilizotukuka zinaendelea kuiongoza nchi kujipatia mafanikio zaidi.



## Vijana washauriwa kujiunga vyuo vya kati

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amewataka vijana mkoani humo kujiunga na vyuo vya kati ili kupata ujuzi utakawasaidia kupata ajira kwenye shughuli mbalimbali za kujenga makao makuu ya nchi.

Alitoa ushauri huo juzi jijini hapa katika mahafali ya tano ya Chuo cha Dodoma Vocational Training Centre (Dodoma VCT).

Aliwataka vijana kuhakikisha wanapata ujuzi ili kuzikimbilia fursa mbalimbali ambazo zitapatikana kutokana na ujio wa serikali Dodoma.

"Wito wangu kwa vijana wa Mkoa wa Dodoma niwatake kuwa na ujuzi katika makao makuu ya nchi niwatake kila mmoja apate ujuzi, tumieni vyuo vya kati wazazi niwaombe watoto wapate ujuzi kama hajafaulu apate nafasi ya kusoma ujuzi wowote, Dodoma na Dunia tunayoiendea itakuwa na fursa nyingi, lakini kama huna ujuzi utapishana na fursa," alisema Mtaka.

Vilevile, alisema kuwa hivi sasa Dodoma ni Makao Makuu hivyo vijana hawana budi kujiandaa ili miradi inayokuja iwakute na ujuzi.

"Hapa ujenzi ni mkubwa sana kama unakaa nyumbani hakuna kibarua ni wewe tu, tumia fursa tunajenga hapo Msalato kiwanja cha ndege kikubwa kabisa wakikuuliza una ujuzi wewe upo tu huna unachojua tafuta ujuzi wowote," alisema.

Alikitaka chuo hicho kuongeza ubunifu pamoja na kozi mbalimbali ili watu wengi wapate ujuzi ambao utasaidia kuondokana na tatizo la ukosefu wa ajira.

"Mkuu wa chuo nakushauri sana ongeza kozi tujitahidi tuweke matangazo kwamba chuo kinafundisha kozi hizi na hizi uwaokoe watoto wa Dodoma, tunataka vijana wa mkoa huu wawe washindani tuwapeleke kwenye elimu zote," alisisitiza Mtaka.

Pia, aliwataka wanafunzi licha ya kujifunza masomo mbalimbali pia wanatakiwa kuwa wabunifu ili wanapomaliza masomo yao waajirike.

"Mjifunze vyote ujuzi na ubunifu ukienda mahali kutafuta vibarua unakuwa umekamilika kwa kila kitu, tunapeleka umeme vijiji vyote vya Tanzania kule vijijini hakuna mafundi maana yake fundi ni wewe," alisema.

Awali, akisoma risala Mkuu wa Chuo hicho, Jemima Nchimbi, alisema wanakabiliwa na tatizo la kukosa eneo la kujenga chuo kutokana na walilonalo hivi sasa kuwa na mgogoro.

Hata hivyo, alisema kero nyingine ni vijana kutopata mikopo kwa kozi za ufundi stadi na uelewa mdogo wa wazazi kuhusu kozi zinazatolewa na chuo.

# Kituo cha umeme Zuzu kukamilika Septemba

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UJENZI wa kituo cha kupoza umeme cha Zuzu jijini hapa, unatarajiwa kukamilika Septemba mwaka huu.

Miongoni mwa kazi za kituo hicho ni kupokea umeme kutoka Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere na kupeleka maeneo ya kaskazini mwa nchi kupitia Singida na maeneo ya Kusini kupitia Iringa.

Akizungumza jana kwenye ziara ya viongozi kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Nishati na Shirika la Umeme nchini (TANESCO), Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Kheri Mahimbali, alisema ujenzi huo ni utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme (Backbone) awamu ya pili.

"Tumekamilisha ile ziara ambayo tumeanza nayo ambapo tumeangalia tutakavyoutoa umeme kutoka Julius Nyerere mpaka Chalinze na kutoka Chalinze mpaka Dodona, kwa ujumla sisi tumefarijika kuwapata viongozi kuja kutembelea ni wadau muhimu kwetu," alisema.

Naye Mhandisi Mkuu kutoka TANESCO Dodoma, Donasiano Shamba, alisema wamenufaika na mradi huo kwa kuwa utaongeza megawati za umeme.

"Mkoa wa Dodoma tumenufaika sana na mradi huu huko nyuma tulikuwa na megawati 34 ina maana transfoma zilizokuwapo zilikuwa ni mbili ambazo capacity (uwezo) yake ilikuwa jumla ni megawati 32, lakini baada ya mradi huu ambao umeongeza transfoma mbili kila moja ilikuwa na uwezo wa megawati 100 hivyo tumekuwa na megawati 200," alisema.

Alisema miaka ya nyuma umeme wa Mkoa wa Dodoma haukuwa katika hali nzuri, lakini baada ya kuongeza transfoma umekuwa vizuri.

"Mwaka 2015 tulikuwa na wateja wachache, lakini baada ya serikali kuhamia Dodoma wananchi wameongezeka sana sasa hivi tuna wateja zaidi ya 160,000 yote sababu ya uwepo wa kituo hiki inatupa uwezo wa kuendelea kuwahudumia wananchi," alisema.

Naye Mratibu wa Mradi wa kituo cha kupoza umeme Zuzu, Mhandisi Peter Kigadye, alisema kuwa ujenzi wa njia kuu ya kusafirisha umeme (Backbone) awamu ya pili, unagharimu Dola za Marekani milioni 54.3 pamoja na kituo cha mkoani Singida.

Kamishna wa Fedha za Nje kutoka Wizara ya Fedha na Mipango, Sauda Msemo ambaye aliwakilisha Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, alisema viongozi hao wameridhishwa na jinsi mradi huo unavyotekelezwa.

"Sisi Wizara ya Fedha na Mipango na wenzetu wa Wizara ya Nishati na TANESCO tutaendelea kushirikiana ili kuhakikisha tunafikia malengo kwa mafanikio makubwa," alisema.

Alisema wamefika katika kituo hicho ili kuona hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi na kuwa na uwezo wa kupokea umeme wa kiwango kinachotakiwa.

"Huu ni mwendelezo wa ziara tulianzia katika Bwawa la Mwalimu Nyerere tukafuatiwa na Kinyerezi kisha Chalinze kuona zile substation (vituo vya umeme) kwa hiyo ni mwendelezo ilikuwa na lengo la kuona miradi hii na hatua ambazo zimechukuliwa," alisema.

Kamishna huyo alisema Wizara ya Fedha itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya miradi mbalimbali ambayo ina manufaa kwa nchi.



Mnunuzi wa nafaka na msafirishaji wa kampuni ya Madinda Store, Madinda Chibago, akipima mtama kwenye mizani kwa ajili ya kuhifadhi kwenye mifuko, baada ya kununua kutoka kwa wakulima, mkoani Dodoma hivi karibuni. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Unyanyapaa chanzo vijana kutofika vituo vya afya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MIONGONI mwa sababu zinazosababisha vijana hususan wa kike wanaoishi na virusi vya Ukimwi (VVU), kutofika kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ni ubaguzi na unyanyapaa dhidi yao, imeelezwa.

Mtaalamu wa Masuala ya Jinsia na Maendeleo ya Jamii, Dk. Katanta Simwanza, aliyasema hayo juzi katika mafunzo ya wataalamu wa afya, Maofisa Maendeleo ya Jamii na Maofisa wa Habari wa Halmashauri kutoka mikoa mitatu ya Lindi, Mtwara na Pwani.

Mafunzo hayo yameandaliwa na Tume ya Kudhibiti UKIMWI (TACAIDS) kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia uwezeshaji wa Wanawake (Un Women) kwa ufadhili wa mfuko wa Global (Global Fund).

Akizungumza kwenye mafunzo hayo, Dk. Simwanza alisema utafiti unaonyesha kuwa kundi la vijana wenye umri wa kati ya miaka 15 hadi 24 lipo hatarini kupata maambukizi mapya ya VVU.

Hata hivyo, alisema kundi hilo halitaki kwenda katika huduma vituo vya kutolea huduma kwa kuogopa kunyanyapaliwa.

"Pale anapokwenda kituo cha afya hasa kupata huduma za VVU na uzazi wa mpango, jamii inawauliza wewe bado ni mtoto mdogo unakujaje hapa, hizi kauli na nyingine zinawasababisha wasifike kwenye vituo," alisema.

Mtaalamu huyo alisema masuala hayo yanasababisha rika hilo kutovunja ukimya kuhusu VVU na kuitaka jamii kuondokana na dhana hiyo.

Naye Mratibu wa Jinsia katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mwajina Lipinga, alisema mafunzo yatawasaidia maofisa na watendaji wa serikali kujenga chachu ya kupunguza mila na desturi ambazo zinaleta madhara kwa jamii.

Mratibu wa Ukimwi na Mwitikio wa Jamii Wilaya ya Bagamoyo, Grace Tete, alisema ngoma za unyago zinazofanyika usiku ni miongoni mwa vyanzo vinavyochangia maambukizi mapya ya VVU kwa kundi hilo.

Alishauri ngoma hizo kuchezwa mchana ili kusaidia kupunguza maambukizi hayo.



# RC aagiza msako wizi wa dawa nyumba kwa nyumba

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amewaagiza wakuu wa wilaya zote za mkoa huo kuunda kamati maalumu za kuchunguza dawa za serikali zinazouzwa kwenye maduka ya watu binafsi na wahusika wachukuliwe hatua za kisheria.

Homera alitoa maagizo hayo juzi alipofanya ziara ya kusikiliza kero za wananchi katika maeneo mbalimbali ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

Alisema kumekuwa na tabia ya baadhi ya watumishi wa afya kutorosha dawa za serikali hospitalini na kuziuza kwenye maduka ya watu binafsi.

Vitendo hivyo, alisema vinaisababishia serikali hasara kubwa pamoja na kufanya kuwapo uhaba wa dawa kwenye vituo vya serikali vya kutolea huduma za afya hali. Pia alisema inayosababisha manung'uniko miongoni mwa wananchi.

Katika kusikiliza kero hizo, wananchi wengi walilalamika kuwa wamekuwa wakienda hospitalini kutibiwa lakini mara kwa mara wanaandikiwa dawa na kutakiwa kwenda kununua kwenye maduka ya watu binafsi kutokana na dawa hizo kutokuwapo kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Alisema msako huo utafanyika mpaka kwenye makazi ya watumishi wa afya na kwamba hata kama kuna mtu atakuwa amezificha zichukuliwe na yeye kuchukuliwa hatua za kisheria.

"Hili tatizo la dawa limekuwa kubwa na ni la nchi nzima. Pia limekuwa likisababishwa na watumishi wa afya wasiokuwa waaminifu ambao wamekuwa wakiiba dawa na kwenda kuziuza kwenye maduka ya watu binafsi," alisema na kuongeza:

"Wako baadhi dawa za serikali zikiletwa wanasema 'mgodi umetema'. Nawahakikishieni tutafanya upekuzi duka kwa duka ili wahusika wakamatwe. Lakini kwenye nyumba za watumishi wa afya tutafanya upekuzi nyumba kwa nyumba na kitanda kwa kitanda."

Hata hivyo, Homera aliwataka wananchi kutochanganya maduka ya watu binafsi na maduka ya Bohari ya Dawa ya Taifa (MSD) kwa maelezo kuwa maduka ya MSD ni ya serikali na yanatakiwa kupatikana ndani ya hospitali.

Pia aliagiza kila kituo cha serikali cha kutolea huduma za afya kuwa na dirisha maalumu la kuhudumia wazee ili kuwaepushia kukaa muda mrefu wakisubiri huduma.

Awali, baadhi ya wananchi, wakiwamo wazee, walidai kuwa wamekuwa wakifika hospitalini kupata huduma za afya lakini wanaambiwa dawa hazipo na kutakiwa kwenda kuzinunua hali ambayo walidai ni kero kwao.

Mmoja wa wazee hao, Hezron Mwaikenda, alisema walishaambiwa kuwa wazee watakuwa wanatibiwa bure lakini kwa sasa hali haikuwa hivyo kutokana na dawa kukosekana hospitalini, hivyo kulazimika kwenda kununua. "Mimi nina kadi ya kutibiwa bure, lakini nikifika hospitalini naandikiwa dawa ili nikazinunue kwenye maduka. Sasa huwa nashindwa kuelewa kwamba huu utaratibu ndio wa aina gani," alisema Mwaikenda.

Naye Diana Mwaigomole alisema hata watoto wa umri wa chini ya miaka mitano matibabu yao sasa hivi ni gharama kwa madai kuwa wanatakiwa kununua dawa.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akiwahutubia wakazi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya juzi, wakati wa mkutano wa kusikiliza kero. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Aomba ushirikiano kutokomeza uhalifu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI mkoani Mbeya wametakiwa kuendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi kukabiliana na uhalifu kwa kutoa taarifa mapema wanapobaini uwapo wa vikundi vya wahalifu kupanga njama za kutekeleza vitendo hivyo kwenye maeneo yao.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulric Matei, alisema hayo juzi alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari huku akibainisha kwamba kwa sasa uhalifu umepungua kwa kiwango kikubwa mkoani hapa.

Alisema katika miezi ya karibuni, viliibuka vikundi vya watu vilivyokuwa vinavamia waendesha pikipiki na kuwajeruhi kisha kuwapora pikipiki zao, lakini kutokana na ushirikiano kati ya jeshi na wananchi, vikundi hivyo visambaratishwa.

Kwa mujibu wa Matei, baadhi ya wahusika walikamatwa na kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwamo kufikishwa mahakamani na kwamba mpaka sasa walishafungwa na wako jela.

"Jeshi la Polisi tuko makini, hakuna uhalifu ambao utafanyika tusijue. Tunachohitaji ni wananchi kuendelea kutupatia ushirikiano ili kuendelea kuufanya mkoa wetu kuwa shwari na wananchi wafanye kazi zao kwa uhuru," alisema Matei.

Alisema kwa sasa wanaendelea kuimarisha ulinzi na usalama ili serikali itakaporuhusu wananchi kufanya biashara usiku na mchana iwe rahisi kusimamia jambo hilo.

Pia alisema jeshi hilo linaendelea kudhibiti ajali za barabarani kwa kutoa elimu kwa makundi mbalimbali ya wananchi wakiwamo wamiliki wa magari, madereva na wadau wengine wa usafirishaji ili nao washiriki kuzuia ajali kupitia kaulimbiu ya 'Mbeya Bila Ajali Inawezekana'.

Alisema katika maeneo ya miteremko mikali wanaendelea kusimamia utaratibu wa magari ya abiria na ya mizigo kupita kwa awamu ili kupunguza madhara kwa binadamu inapotokea ajali.

# Mbunge aiangukia serikali ujenzi wa mitaro

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, ameiomba serikali kuharakisha ujenzi wa mitaro ya maji kwenye barabara kuu ya Tanzania na Zambia (TANZAM) ili kuwaepusha wananchi na mafuriko yanayoweza kusababisha maafa pindi mvua itakapoanza kunyesha.

Njeza alitoa ombi hilo juzi kwenye mkutano wa hadhara wa kusikiliza kero za wananchi ulioitishwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera na kufanyika katika Uwanja wa Mahubiri.

Alisema wananchi wanaoweza wakaathirika zaidi na mafuriko hayo endapo mitaro haitaimarishwa katika Kata ya Nsalala ambao wako eneo la bondeni kuliko maeneo mengine.

Alisema katika kata hiyo, wananchi wamekuwa wakipata shida ya mafuriko kwa muda mrefu, lakini safari hii hali inaweza kuwa mbaya zaidi endapo mifereji hiyo haitaimarishwa.

"Tunawaomba Wakala wa Barabara (TANROADS) watusaidie kuboresha mitaro hii mapema kabla mvua haijaanza kunyesha vinginevyo nyumba za watu zitakuja zibomoke na kuna uwezekano watu wakapoteza maisha," alisema Njeza.

Pia aliiomba serikali kutekeleza ahadi za kuboresha barabara katika mji huo ambazo ni ahadi ya aliyekuwa Rais, Hayati John Magufuli, alizozitoa mwaka 2019 alipokuwa ziarani mkoani hapa.

Alisema Magufuli aliahidi kujenga barabara za lami zenye urefu wa kilomita 30 pamoja na kuunganisha mji huo na miji mingine kwa barabara za lami ikiwamo barabara ya Mbalizi -Mkwajuni na Mbalizi-Shigamba.

Alisema wilaya hiyo ina barabara nyingi ambazo ni za kimkakati kutokana na kutumika na wananchi kusafirisha mazao kutoka mashambani kwenda sokoni.

Naye Mwenyekiti wa Kitongoji cha Tunduma Road, Adam Mselebende, alisema katika mji huo maji yamekuwa yakisumbua kutokana na makandarasi kufukia mifereji ya maji. Alisema wako pia baadhi ya wananchi wamekuwa wakiharibu miundombinu hiyo kwa kutupa taka ovyo hali ambayo husababisha mitaro kuziba wakati wa mvua.

"Tatizo hili ni kubwa sana kwetu wananchi wa Tunduma Road. Mvua ikinyesha maji yote yanakuja kwetu hata barabara huwa hazipitiki kabisa. Sasa tunaomba sana watusaidie angalau sasa hivi naona wanaendelea kujenga lakini tunaomba waimalize," alisema Mselebende.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Steven Katemba, alisema mapato ya halmashauri hiyo asilimia 80 yanategemea ushuru wa mazao ya kilimo, hivyo akaomba barabara ziendelee kuboreshwa ili wasafirishe kirahisi.

Alisema baadhi ya barabara, ikiwamo ya Inyala-Simambwe, ambayo inajengwa kwa kiwango cha lami imepita kwenye mashamba ya wananchi, hivyo akadai kuwa zitasaidia kurahisisha usafirishaji wa mazao hayo.

Katika eneo hilo, alisema wananchi wanazalisha viazi, mahindi, mboga na matunda na kwamba baadhi ya mazao hayo yanahitaji usafiri wa uhakika ili yasiharibike.



## Ataka utafiti kusaidia jamii

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MKUU wa Mkoa wa Kusini Pemba amewataka wanafunzi kuendelea kusoma masomo ya sayansi na kufanya utafiti mdogo na kuziteremsha kwa jamii ili kutoa matokeo chanya yanayoweza kuibadilisha kutokana na rasilimali zilizowazunguka.

Mattar Zahor Massoud aliyasema hayo kwenye Ukumbi wa Shule ya Sekondari ya Madungu alipozungumza na wanasayansi wachanga baada ya kukagua maonyesho mbalimbali ya kazi zao.

Alisema pamoja na utafiti mdogo uliofanywa na baadhi ya wanafunzi wa shule za sekondari kisiwani Pemba, lakini una maana na umuhimu mkubwa kwa vile umeteremka kwa jamii moja kwa moja kutokana na uhalisia wake.

Alisema hao wanafunzi ambao ni wanasayansi wachanga Tanzania, wamefanya kazi ambayo ni muhimu na inaleta taswira kubwa kwamba wanafunzi wakiendelezwa wana uwezo wa kubuni vitu vikubwa na baadaye kutegemewa katika kuiletea maendeleo nchi yao.

"Endeleeni na washawishini wenzenu kusoma masomo ya sayansi, epukaneni na kauli ya kuwa masomo hayo ni magumu kwa kuwa ni kinyume cha wanavyofikiria," alisema.

Alisema siyo lazima kusubiri watafiti kutoka nje ya nchi kwa kuwa hata wanafunzi wanapaswa kujifunza wao wenyewe kwa kusaidiana na walimu wao ili mwisho wa safari nao kujulikana.

Kiongozi huyo alisema serikali itaendelea kuunga mkono juhudi zinazochukuliwa na taasisi ya Young Scientists Tanzania, ili kuibua vipaji vya wanafunzi kama hao na wanasayansi tegemeo kwa siku za baadaye.

"Tunapaswa kufikiria nini cha kufanya ili kuondokana na utegemezi wa kitaaluma na wavumbuzi kutoka nje kila mara," alihimiza.

Aliishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kuangalia namna ya kuboresha mitaala ili kutoa fursa ambazo zitawawezesha wanafunzi kuvumbua mambo yatakayolisaidia taifa.

Alitaja utafiti uliofanywa na wanafunzi hao ukiwamo wa kutumia mawe makubwa kwa ajili ya kilimo cha mwani ili kuepusha ukataji wa miti kwa ajili ya kilimo hicho, jambo litakalosaidia udhibiti wa uharibifu wa mazingira.

Ofisa Mipango wa wizara hiyo, Mussa Khamis Mussa, aliipongeza Taasisi ya Young Scientists Tanzania kwa kuwashajihisha wanafunzi hao kuwa wabunifu wa vitendo kwa kufanya utafiti wa kujenga jamii.

Mratibu wa Taasisi hiyo Zanzibar, Ame Haji Vuai, alisema taasisi hiyo ilianza zamani, lakini umaarufu kwa Zanzibar ulijitokeza mwaka 2011, ikiwa na lengo la kutumia taaluma na utafiti kutatua kero za kijamii.

Alisema lengo lingine la kuanzishwa taasisi hiyo ni kuwashajihisha wanafunzi kupenda kusoma masomo ya sayansi ili kutatua kero zao ikiwamo ya ajira.

## BAA LA CORONA

# Waziri: Jiandaeni kwa chanjo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, amewataka wananchi kutobabaishwa na taarifa zinazosambazwa katika mitandao ya kijamii kuhusu chanjo ya corona na badala yake kujiandaa kupata chanjo hiyo.

Aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari nje ya kongamano la kutathmini kazi za uuguzi na ukunga katika Ukumbi wa Shekhe Idrisa Abdulwakil ulioko Kikwajuni, Zanzibar.

Alisema mitandao ya kijamii na baadhi ya viongozi wamekuwa wakipotosha kuhusu chanjo hiyo na kudai kuwa ina madhara, jambo ambalo si la kweli.

Waziri huyo aliwataka wananchi wasidanganyike kuhusu chanjo hiyo, akidai haina madhara na ni nzuri kwa afya zao.

Alisema utoaji wa chanjo hiyo unaendelea vizuri kwa wahudumu wa afya na wafanyakazi wa viwanja vya ndege na bandari na baada ya hapo itashuka kwa wananchi, wakitarajia kuanza na kundi la wazee na wagonjwa wa kisukari.

Alisema Serikali ya Zanzibar inatarajiwa kupokea msaada ya chanjo zingine 100 ili kuwakinga wananchi na ugonjwa wa corona.

Alisema suala la utoaji wa chanjo siyo geni na kutolea mfano chanjo ya ugonjwa wa ndui ambapo wananchi wengi walifariki dunia kutokana na ugonjwa huo, lakini baada ya kutolewa kwa chanjo ugonjwa huo ulitoweka.

Alisema chanjo ya corona itatolewa bure kwa wananchi hivyo wananchi wajiandae kuipokea chanjo hiyo.

Waziri huyo alibainisha hadi sasa hakuna kifo kilichotokea kutokana na corona katika wimbi la tatu la ugonjwa huo na kwa sasa kuna wagonjwa wanane ambao wanaendelea kupatiwa matibabu.

"Wagonjwa wanane, watatu ni wanawake na watano ni wanaume na tayari mgonjwa mmoja katika ya hao wanane tayari ameshapata ruhusa na waliobakia wote hao hali zao za kiafya zinaendelea vizuri," alisema.

Waziri huyo aliwataka wananchi kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo na kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya katika kujikinga na corona ikiwamo kuvaa barakoa na kuepuka mikusanyiko isiyo ya lazima.

Hivi karibuni, Ofisi ya Mufti Zanzibar iliandaa kongamano la viongozi wa dini na kutoa tamko la kuwataka wananchi kuchanja chanjo ya corona ikiwa ni hatua ya kuchukua tahadhari.




Mkuu wa Mkoa wa Kusini Pemba, Mattar Zahor Massoud, akizungumza na wanasayansi vijana, baada ya kuangalia maonyesho yao katika Shule ya Sekondari Madungu, Pemba jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwinyi aona kielelezo Muungano kudumishwa

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema uwapo wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere visiwani Zanzibar, ni kielelezo chanya katika kuenzi na kudumisha Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa vitendo.

Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, alibainisha hayo jana aliposoma hotuba kwa niaba ya Rais Dk. Mwinyi katika hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi kwenye mradi wa ujenzi wa mabweni ya wanafunzi wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere – Kampasi ya Karume, Zanzibar.

Alisema bodi pamoja na uongozi wa chuo hicho wamekuwa wakifanya kazi nzuri na tangu kuanzishwa kwa chuo hicho mnamo mwaka 1961 mpaka sasa, chuo kimekuwa kinaishi kwa mawazo ya waasisi wa Taifa la Tanzania, Hayati Mwalimu Nyerere na Karume.

Makamu wa Pili wa Rais alisema kutokana na jitihada mbalimbali zinazochukuliwa na uongozi wa chuo hicho, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar inatambua mchango unaotolewa na chuo hicho katika kutoa mafunzo mbalimbali kwa ngazi ya cheti, stashahada, shahada na shahada ya uzamili.

Mbali na utoaji huo wa mafunzo, Hemed alisema chuo kina mchango mkubwa katika kutoa mafunzo ya uongozi, maadili na uzalendo kwa wanafunzi na watumishi mbalimbali ambao kwa namna moja au nyingine wanasaidia katika kutekeleza majukumu yao kupitia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

Alisema ni ukweli usiopingika wahitimu wanaotoka katika chuo hicho baada ya kumaliza mafunzo yao, hutoka wakiwa wameiva, wenye uadilifu na weledi wa hali ya juu, jambo ambalo lina umuhimu kwa watu ambao hupewa dhamana katika nafasi za utumishi wa umma.

"Tangu kuanzishwa kwa chuo hiki, kimewanufaisha Watanzania wengi na serikali kwa ujumla, kupitia chuo hiki kimepata wahitimu wengi wenye ari na bidii ya kulitumikia taifa hili kwa weledi na kuchangia katika maendeleo ya taifa," alisema Makamu wa Pili wa Rais.

Alisema kitendo cha chuo hicho kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa mabweni ya wanafunzi kinaashiria kutekeleza kwa vitendo mipango ya serikali kwa kuzingatia maelekezo ya serikali kupitia Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia ikiwamo suala kuongeza udahili wa wanafunzi na ujenzi wa miundombinu mbalimbali katika taasisi za kielimu.

"Niwasihi wadau wote wa maendeleo mliopo hapa mtuunge mkono katika ujenzi wa mabweni haya ambayo yatagharimu Sh. 15 na kukamilika kwake kutasaidia sana wanafunzi kupata malazi bora na salama na hatimaye kuwapatia ari ya kusoma ili kupata maarifa bora yatakayoongeza maendeleo kwa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla," alisema.

Alimwomba mkandarasi wa mradi huo ambaye ni SUMA JKT kukamilisha mradi huo kwa wakati uliopangwa na mradi huo unalenga kutatua kero kubwa iliyopo kwa wanafunzi kukosa makazi.

Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohamed Said, alipongeza uongozi wa Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere kwa kuhakikisha yale malengo waliojiwekea ya kutoa mafunzo ya uongozi na uzalendo kwa jamii yanafikiwa.

Simai aliukumbusha uongozi wa chuo hicho mbali na mafunzo ya uongozi na uzalendo wanayoyatoa, lakini ipo haja ya kuangalia upya uwezekano wa kuwafanya wanafunzi wawe na uwezo wa kufanya vitu vingi kwa pamoja kwa kuzingatia masuala ya ubunifu na uvumbuzi kama zinavyofanya nchi zingine duniani.

Mkuu wa Chuo hicho, Profesa Shadrack Mwakalila, alitumia fursa hiyo kumshukuru na kumpongeza Rais kwa jitihada anazoendelea katika kukuza uchumi wa Zanzibar.

Profesa Shadrack alisema chuo hicho kimeamua kuingiza somo la uongozi na uzalendo katika kila kozi ili kuwajenga wanafunzi wanapomaliza mafunzo yao ili kuwajenga vijana kuwa viongozi bora na wenye weledi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

### KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

**ISSA MOHAMED MKOMELA** anatangaza kupotelewa na kadi za pikipiki aina ya **BAJAJ BOXER BM 125-X** zifuatazo,kadi yenye namba za usajili **MC 136 CFD** chasis namba **MD2A21BYXKWM88391** engine namba **JF2WK85389,** na kadi yenye namba za usajili **MC 152 CJM chasis namba MD2B15BYIKWE92689** engine namba **JV2WKE44053,** yoyote atakayeziokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa

**DAR/CEN/RB/363809/2021**

116374502

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUGU PEARSON RUGAMBWA NDYAKOWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T697CQS** aina ya **TOYOTA NOAH** yenye Chasis No. **SR400207462,** Engine **No. 357877973.**

Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu. Taarifa ya Polisi namba

**GE/TR/RB/3415/2021**

116375302

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MWENDI MZIWANDA MWESONGO** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 172 BBT** – TOYOTA HILUX. YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **ARU/ARU/RB/364396/2021.**

116375402

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MATHEW PAULO KIMARIO** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 835 ACT.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.

T AARIFA YA POLISI: **ARU/ARU/RB/880109/2020.**

116375502

### KUPOTEA KWA HATI YA NYUMBA

**MATHIAS RAPHAEL GINGI** anatangaza kupotelewa na hati ya Nyumba **9184-DLR PLOT No. 36 BLOCK 'A' KIKUYU SOUTH HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA.**

yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi kilichopo karibu yake. Taarifa ya polisi.

**DOD/DOD/RB/51201/2021.**

116375602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Baruapepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaa wa Moshi,**
**S.L.P 2888,**
**40470 DODOMA**
**Tarehe 27-07-2021**

### TAARIFA KWA UMMA

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **ALHAMISI tarehe 29-07-2021** Kampuni ya **FAMARI INVESTMENT** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DAR ES SALAAM kuelekea TUNDUMA** gari hilo lenye namba za usajili **T 592 DQU / T 281 DBV**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **21** |
| **Upana** | - | **mita** | **3.4** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.1** |

3. Njia itakayotumika: **DAR ES SALAAM hadi TUNDUMA kupitia VIGWAZA/-MAKAMBAKO**

***Gari itasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

116376102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika mahakama ya Mwanzo ya Wilaya DODOMA MJINI**

**Kituo cha CHAMWINO MJINI Mkoa DODOMA.**

**Usimamizi wa mirathi Na.30/2021.**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU MUSSA JUMA GWANDI WA MAILIMBILI DODOMA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA MARIAM MOHAMMED SHABANI**

**TANGAZO**

(Kanuni ya 5(2) ya kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na Mirathi ya Marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 04 mwezi 08 mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

**Zingatia;** Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

**Imetolewa leo tarehe 26 mwezi 07 mwaka 2021.**

116375702

**KABANGO GENERAL BUSINESS (T) LTD**

**SHAURI NAMBA 659/2020**
**PAMOJA FINANCIAL SERVICES...............MDAI**
**DHIDI YA**
**AYUBU JUMA AYUBU................MDAIWA**

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa amri na idhini tuliyopewa na Baraza la ardhi na nyumba Wilaya ya Kinondoni inayotuamuru kuuza eneo lililoko Boko cha Chui Wilaya ya Kinondoni Dar es salaam kwa njia ya mnada tarehe 09/08/2021 saa tano kamili asubuhi, mnada utafanyika mahali eneo lilipo.

**MASHARTI YA MNADA**

Mnunuzi atakayeshinda katika mnada atatakiwa kulipa 25% papo hapo kwa bei itakayofikiwa na 75% zitalipwa ndani ya siku kumi na nne (14), mnunuzi akishindwa kulipa kiasi kilichobaki ndani ya siku kumi na nne (14) pesa iliyotolewa haitarudishwa na mnada utarudiwa.

**Kwa Mawasiliano zaidi wasiliana nasi kwa namba zifuatazo hapo chini: 0788 026933 / 0713 024068.**

116376002

### KUPOTELEWA NA HATI YA KIWANJA

**ANTHONY NELSON KAFUGUGU** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA HATI YA KIWANJA **PLOT NO 1499** NA **1501 BLOCK R MBULU** KAHAMA YENYE **CT NO 74780.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.

116376402

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**JOHN SLIVASTA MOLWA Wa Nyashinbi mjini Kahama, anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC.247 CUF.**

**Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake,**

**Taarifa ya jeshi la polisi, KAH/RB/TR/380/2021.**

### KUPOTEA KWA CHETI



116375202

**YAHYA SALUM ALLY** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S 5380/0044 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary **JBUN JAZAR ISLAMIC** mwaka **2018,**yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Polisi taarifa **DAR/CEN/RB/ 348959/2021**




TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## MAKALA MAALUM

# Mauaji wivu wa mapenzi yanavyoacha simanzi -3

## ●Polisi, LHRC na wanasaikolojia wanena

Na Maulid Mmbaga

**SEHEMU ya pili ya ripoti hii, iliendelea kuangazia idadi ya matukio ya mauaji, na kuonyesha mengi sababu ikiwa ni wivu wa mapenzi, kwa kipindi cha mwaka 2020 hadi Julai 2021. Endelea...**



Septemba 17, Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Singida ilimhukumu kifungo cha miaka 30 jela mkazi wa Mtaa wa Kipungua mkoani humo Hamis Mtanda (37) baada ya kukutwa na hatia ya kumbaka mtoto wake wa kumzaa (11), baada ya kuachana na mama yake.

Septemba 22, watu wasiojulikana waliwajeruhi kwa mapanga watu watatu Kisiwani Pemba, wakiwa wanasali alfajiri na chanzo cha tukio hilo hakikubainishwa.

Septemba 24, mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Kiaga, mkoani Mara, alishikiliwa na polisi baada ya kumkata mapanga mwalimu wake Majogoro John, na kumsababishia majeraha, baada ya kuamriwa akaite wazazi kwa sababu ya utoro shuleni.

Siku hiyo pia, TAKUKURU wilayani Ikungi, mkoani Singida ilimshikilia mfanyabiashara Ashrafal Mohamed (51), kwa tuhuma za kumbaka na kumweka kinyumba mwanafunzi wa kidato cha pili.

Septemba 26, mkazi wa jijini Dar es Salaam Ombeni Alfayo, alishikiliwa na polisi jijini hapo kwa tuhuma za kumkata kiganja mkewe, sababu wivu wa mapenzi.

Septemba 27, Polisi Mkoa wa Manyara liliwashikilia watu saba kwa tuhuma za kumuua kikatili Manase William (47) aliyekuwa mlinzi wa mgodi wa Bilionea Saniniu Laizer, chanzo cha mauaji hayo hakikubainishwa.

Septemba 28, Meckrida Masesa (25) mkazi wa Kahama, alituhumiwa kwa kudaiwa kumchoma moto na kumsababishia majeraha mdogo wake kwa madai ya kumchukulia mumewe.

Septemba 30, watu wanne walifikishwa mahakamani kwa tuhuma za kumuua, Emmanuel Mlelwa mkazi wa Jombe, chanzo hakikubainishwa.

Oktoba 4, Samson Kyando (26), mkazi wa mkoani Mbeya, alituhumiwa kwa kumuua mkewe Cecilia Wilison (24) kwa kumchapa na fimbo hadi kufa, chanzo ugomvi wa kifamilia.

Polisi mkoani Rukwa, ilimshikilia Stella Kangoza (29) mkazi wa Sumbawanga, kwa tuhuma za kumchoma moto mwanawe mikononi, mwanafunzi wa darasa la tatu kwa madai ya kuiba Sh. 400 za sadaka.

Oktoba 11, polisi mkoani Shinyanga lilimshikilia Paulo Shija (30) kwa tuhuma za kumuua mkewe Mariam Julias (26) kwa kumchoma na kisu shingoni sababu ni wivu wa mapenzi.

Aidha, Ramadhani Yusufu (22) alihukumiwa kifungo cha maisha baada ya kukutwa na hatia ya kumlawiti mtoto wa kike wa shemeji yake (3).

Oktoba 12, polisi mkoani Shinyanga, liliwashikilia vijana wawili kwa tuhuma za kumbaka mtoto mwenye umri wa miaka sita kwa zamu.

Oktoba 13, Polisi Mkoa wa Dodoma, lilimshikilia Daniel Massawe (40) kwa tuhuma za kumjeruhi kwa risasi mkewe, kwa madai ya wivu wa mapenzi.

Oktoba 15, watu wawili waliuawa kwa kushambuliwa na watu wasiojulikana, katika Manispaa ya Morogoro, na chanzo kikitajwa ni mgogoro wa shamba.

Oktoba 17, mtoto Rahel Yohana (14), mkazi wa mkoa wa Morogoro, alikutwa porini akiwa amejinyonga baada ya kukaripiwa na mama yake.

Siku hiyo hiyo, polisi mkoani Kagera lilimshikilia Frodius Protace (24), kwa tuhuma za kujifanya daktari na kumtoa mimba Saraiya Idd (25) na kumsababishia kifo.

Oktoba 18, vijana 10 walituhumiwa kwa kumchoma moto mama yao wa kambo, Daines Mdee (26), wakimtuhumu kutumia hati za nyumba zao za urithi kuchukulia mkopo benki.

Pia Jeshi la Polisi mkoani Mbeya, liliwashikilia watu watano kwa tuhuma za kumuua baba yao mzazi, kutokana na ugomvi wa mashamba.

Oktoba 22, Polisi mkoani Mwanza liliwashikilia watu wanne kwa tuhuma za kukeketa mtoto wa siku tisa.

Oktoba 29, Faraja Yunus (44) mkazi wa mkoani Kagera alituhumiwa kwa kosa la kuwauwa mke wake na shemeji kwa shoka, kutokana na wivu wa kimapenzi.

Novemba 5, mwalimu wa Shule ya Msingi ya Montfort Eneza Anderson (27) alishikiliwa kwa kosa la kumbaka mwanafunzi wake wa darasa la tano, jina limehifadhiwa.

Novemba 8, Juma Ngozi (25) alishikiliwa kwa madai ya kumuua mgoni wake, Abdallah Raisi, kwa madai ya usaliti.

Siku hiyo hiyo, Kurwa Langi (50) mkazi wa mkoani Tabora, alituhumiwa kwa kosa la kumuua mpenzi wake wa zamani Kumbi Shija, kwa madai kuwa amemloga ashindwe kufanya tendo la ndoa.

Novemba 13, Ikonga Chacha, mkazi wa mkoani Mara alihukumiwa kifungo cha miaka 12 jela baada ya kupatikana na hatia ya kumkata kidole Tatu Iddi aliyekuwa akimdai Sh. 23,000.

Novemba 15, mwili wa askari wa kikosi cha Valantia Zanzibar (KVZ) Khalfan Junedi (25), aliyepotea katika mazingira ya tatanisha kipindi cha uchaguzi mkuu, na kudaiwa kuwa aliuawa na watu wasiojulikana.

Novemba 16, watu wawili waliokadiriwa kuwa na miaka 20 na 25 walikutwa wamefariki na miili yao kutelekezwa pembezoni mwa njia katika kijiji cha Mkowale mkoani Ruvuma.

Novemba 18, Polisi mkoani Lindi, lilimshikilia Mbekenyera Ally (23) kwa tuhuma za kumlawiti mtoto mwenye umri wa miaka sita, jina lilihifadhiwa.

Mahakama ya Mkoa wa Wete Pemba, ilimhukumu Mansour Salim Mussa (50) jela miaka mitatu na kulipa faini ya Sh. 200,000, baada ya kukutwa na kosa la kumbaka ndugu yake.

Novemba 22, 2020, Mahakama ya Wilaya Geita ilimhukumu Lugwisha Makungu (20), kutumikia kifungo cha miaka 30 jela naviboko 12, kwa kosala kumbaka mtoto mwenye umri wa miaka 16.

Novemba 26, Mahakama ya Wilaya ya Geita, ilimhukumu Kasonoko Emmanuel (20), kutumikia kifungo cha miaka 60 jela kwa makosa ya kubaka na kumpa ujauzito mwanafunzi wa darasa la sita.

Novemba 30, Mahakama ya Wilaya ya Kigoma, ilimhukumu Agness Damian (40), kifungo cha miaka miwili na kulipa fidia ya Sh. milioni 5, kwa kosa la kumkata kata na wembe mtoto wa mume wake mwenye umri wa miaka 15, kwa madai ya kumpiga mtoto wake.

Desemba 2, Polisi Mkoa wa Pwani, lilimkamata kijana aliyetambulika kwa jina moja Bolizozo, kwa tuhuma za kumuua kikatili Halima Said (50) kwa kumkata mapanga.

Desemba 4, polisi mkoa wa Pwani lilimshikilia Danieli Warioba (43) kwa tuhuma za kumuua mke wake Joyce Ismail (35), mkazi wa Mlandizi.

Desemba 5, mwanafunzi wa darasa la pili katika Shule ya Msingi Chiringe 'B', mkoani Mara, jina lilihifadhiwa, alijeruhiwa na bibi yake kwa kuchomwa na pasi, kwa madai ya kuchana shuka alilokuwa amejifunika.

Desemba 7, polisi mkoani Mwanza, Hamisi Omary (19) mkazi wa Nyasaka Msumbiji,alikamatwa kwa tuhuma za kumuua mwanafunzi wa kidato cha pili katika Shule ya Sekondari Katunguru, Vincent Renatusi (17), na kumwibia vitu vyake.

Desemba 16, Mahakama ya Wilaya ya Lindi, ilimuhukumu Ally Kacha (27) kifungo cha maisha jela, baada ya kukutwa na hatia ya kumbaka mtoto wa umri wa miaka mitatu.

Desemba 22, polisi mkoani Mwanza, lilimshikilia Benson Oluochi (54), kwa tuhuma za kumuua mke wake Elizabert Benson, kwa madai ya kukosa uaminifu ndani ya ndoa.

Desemba 24, polisi mkoani Ruvuma, lilimshikilia askari wake Konstebo Mkwela, kwa tuhuma za kumjeruhi Andrew Milanzi (33) kwa kitu chenye ncha kali kwa kile kilichodaiwa kuwa ni wivu wa mapenzi.

Siku hiyo hiyo mkoani Ruvuma, Neema Athumani (24) mkazi wa Tunduru, alishikiliwa na polisi kwa tuhuma za kumuua mtoto wake Rashfod Tariq (4), kwa kumwekea sumu ya panya kwenye soda na kumnywesha, kutokana na ugumu wa maisha, baada ya mzazi mwenzake kumtelekeza na kukataa kumhudumia mtoto.

**ITAENDELEA KESHO**

# BARCELONA

## Neymar wamalizana nje ya mahakama



**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA wameafikiana na mshambuliaji Neymar Jr kusuluhisha mzozo wao wa kifedha kati yao nje ya mahakama.

Neymar ambaye ni raia wa Brazil mwenye umri wa miaka 29 aliwahi kudai kwamba, Barcelona walikataa kumlipa bonasi ya euro milioni 43.6 alipokamilisha uhamisho wake kwenda Paris Saint-Germain ya Ufaransa mwaka 2017.

Badala yake, Barcelona walifika mahakamani kumshtaki Neymar huku wakidai euro milioni 6.7 ambazo alipata ya baada ya kutia saini mkataba mpya wa miaka mitano mwaka 2016.

Mbali na fedha hizo, Neymar pia alitakiwa kulipia gharama zote nyinginezo ambazo zilitolewa na Barcelona wakati wa mchakato huo wa kisheria.

Juni mwaka 2020, mahakama kuu ya Hispania iliamuru Neymar kuilipa Barcelona fidia ya euro milioni 6.7.

Hata hivyo, fowadi huyo alikata rufani dhidi ya maamuzi hayo ya mahakama na kuishtaki upya Barcelona, ambayo kwa sasa imethibitisha kwamba, wamekutana na Neymar na kupata suluhu ya kudumu nje ya mahakama.

Mapema jana Barcelona ilitangaza kwamba, imefuta kesi yake na sasa wameshafikia makubaliano na Neymar na hakuna mgogoro tena.

Neymar alijiunga na PSG kwa ada ya euro milioni 222, Agosti 2017.

# VAN DIJK KURUDI UWANJANI KESHO DHIDI YA BERLIN

**INNSBRUCK, Austria**




KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amethibitisha kwamba, mlinzi wa kati, Virgil van Dijk atarudi rasmi uwanjani kesho Alhamisi kwenye mchezo wa kirafiki wa maandalizi ya msimu mpya dhidi ya Hertha Berlin.

Van Dijk alicheza katika mechi tano tu na Wekundu hao kwa msimu uliopita na alikosa kuichezea Uholanzi kwenye michuano ya Euro 2020 kutokana kuendelea kujiuguza goti baada ya kuumia Oktoba mwaka jana kwenye mchezo dhidi ya Everton.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 alijumuishwa kwenye kikosi cha Liverpool kilichokwenda nchini Austria kwa ajili ya kambi ya mazoezi mapema mwezi huu, lakini hakutumika kwenye mchezo wa ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Mainz na Klopp aliweka wazi kuwa hana haraka ya kumtumia mlinzi huyo.

Hata hivyo, bosi huyo wa Liverpool yupo tayari kumpa dakika za kucheza Van Dijk pale kwenye dimba la Tivoli Stadion, huku pia mlinzi mwingine wa kati, Joe Gomez - ambaye hajakichezea kikosi hicho tangu alipoumia wakati akiichezea England Novemba mwaka jana, anakaribia kurudi dimbani.

"Natumaini, sina uhakika, kuna nafasi kwa Virgil na anaweza kucheza kwa dakika chache. Anaonekana yupo vizuri kwenye mazoezi na pengine tunaweza kumpa nafasi ya kucheza, lakini nahitaji kuwa na majadiliano ya mwisho. Anaonekana yupo tayari na tutaangalia," alisema Klopp akiiambia tovuti ya Liverpool.

"Kama ukiangalia mechi za sasa kwenye mazoezi, inatia hamasa. Joe anakaribia kurudi dimbani hivi karibuni.

"Hakuna haraka juu ya wawili hao; walikuwa na majeruhi tofauti, lakini wanakaribia sana kurudi uwanjani.

"Kama Virgil anaweza kucheza kwa dakika 20, labda Joey anaweza kucheza kwenye mchezo unaofuata. Tutaona. Kwenye mazoezi wote wapo vizuri kabisa."

# Terry aachana na Aston Villa

**LONDON, England**

ASTON Villa imetangaza kuwa kocha msaidizi, John Terry ameondoka klabuni hapo baada ya miaka mitatu akiwa kwenye timu hiyo chini ya kocha Mkuu, Dean Smith.

Nyota huyo wa zamani wa Cheslea amefikia uamuzi huo kutokana na nia yake ya kutaka kuwa kocha mkuu katika siku zijazo na hivyo atatembelea klabu mbalimbali za Ulaya kujifunza.


"Imekuwa heshima na upendeleo mkubwa kutumikia Aston Villa kwa miaka hii mitatu iliyopita, lakini sasa nahisi ni wakati sahihi kufanya maamuzi magumu kuendelea na mambo mengine," alisema Terry akinukuliwa na tovuti ya klabu hiyo.

Terry mwenye umri wa miaka 40 alitumikia Aston Villa kama mchezaji katika msimu wa 2017/18.

"Nasikitika kumpoteza John kama sehemu ya wakufunzi wangu, lakini naelewa na kuheshimu uamuzi wake," alisema wa mkuu wa Aston Villa, Smith.

Kocha wa Aston Villa, Smith alimtetea Terry kama msaidizi wake, Oktoba mwaka 2018.





# SPURS

## WAJITOSA KUMWANIA RAMSEY

**LONDON, England**

KLABU ya Tottenham Hotspur imejitosa kumwania kiungo wa zamani wa Arsenal, Aaron Ramsey, kwa mujibu wa The Sun.

Juventus wanaangalia uwezekano wa kumuuza nyota huyo wa kimataifa wa Wales ambaye amecheza mechi 46 kwa kipindi cha misimu miwili aliyokaa hapo Turin.

Mkurugenzi wa michezo wa Tottenham, Fabio Paratici anataka kumrudisha Ramsey London ili kuungana na Pierre-Emile Hojbjerg.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Ramsey anaweza kupatikana kwa ada ndogo na atakuwa sehemu muhimu ya kuimarisha safu ya kiungo ya klabu hiyo.

Ramsey awali alikuwa akihusishwa na mpango wa kurudi katika klabu yake ya zamani ya Arsenal, kabla ya dili hilo kiyeyuka.

Pia Liverpool walitajwa kutaka kujitosa kumwania nyota huyo, lakini hakujakuwa na mwendelezo wowote juu ya mpango huo.

Juventus wanataka kumwachia Ramsey ikiwa ni sehemu ya kupunguza bili ya mishahara, ambapo mchezaji huyo ni mmoja wa wanaolipwa mkwanja mrefu hapo kwa kibibi kizee hicho cha Turin.

## MAN CITY BADO WAKOMAA NA KANE



**MANCHESTER, England**

MANCHESTER City imeamua kuendelea na mchakato wa kufukuzia huduma ya Harry Kane kwa muda wote wa dirisha hili la usajili hadi hapo litakapofungwa.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu England wanaamini kwamba, Kane mipango yake ni kuachana na Tottenham Hotspur kwenye dirisha hili la uhamisho wa majira ya joto na kutokana na hilo wanamtaka nahodha huyo wa England atue kwenye kikosi hicho cha kocha, Pep Guardiola.

Matumaini ya Man City ni kulipa ada chini ya Pauni 100 milioni kunasa huduma ya Kane na wanaamini Spurs watakubali akakipige Etihad katika dili litakalohusisha pia kubadilishana wachezaji.

Mwenyekiti wa Spurs, Daniel Levy amezidi kuweka ngumu kwamba nyota wake huyo hauzwi kwa gharama yoyote ile, lakini huko Etihad wao wanaamini dili hilo litatiki tu.

Man City wanaamini matamanio ya Kane kuachana na Spurs yatakuwa rasmi kabla ya dirisha la usajili kufungwa Agosti 31.

Mpango wa miamba hiyo ya Etihad ni kumwona Kane akiongoza kwenye safu ya ushambuliaji ya chama lao mwanzoni mwa msimu ujao, ambapo mechi yao ya kwanza kwenye Ligi Kuu England watakipiga na Spurs, Agosti 15.

Levy hatapenda kuona anawatibua mashabiki wa Spurs kwa kumwona staa wao kwenye jezi za Man City katika mechi yao ya kwanza ya msimu.

# CHELSEA YACHUKUA KIPA BETTINELLI

**LONDON, England**

KLABU ya Chelsea inatarajiwa kukamilisha kumsajili golikipa wa zamani wa kimataifa wa England, Marcus Bettinelli.

Golikipa huyo wa zamani wa Fulham ambaye alikataa ofa kutoka Aston Villa amekubali dili la miaka miwili kuwatumikia mabingwa hao wa Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kwa mujibu wa ripoti za magazeti la England, kipa huyo anatarajiwa kutia saini kwa Blues hao akiwa mchezaji huru baada ya mkataba wake kule Craven Cottage kufikia tamati.

Bettinelli anatarajiwa kukamilisha vipimo vya afya na kutia saini Chelsea chini ya saa 48 zijazo.

Chelsea imekuwa ikisaka golikipa mpya baada ya Willy Caballero kuondoka mwisho wa mwezi uliopita.



## KWA UFUPI

### JUVE KUMBAKIZA RONALDO
KLABU ya Juventus imemweleza Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36 kwamba, wanatarajia abakie klabuni hapo msimu huu. Mshambuliaji huyo raia wa Ureno amekuwa akihusishwa kutaka kutimka wakati huu ambapo mkataba wake ukibakia mwaka mmoja kumalizika. ***(Sky Sports)***

### RAMSEY KUUZWA
JUVENTUS wameonyesha nia ya kumuuza Aaron Ramsey mwenye umri wa miaka 30 msimu huu, na kiungo huyo wa Wales anaonekana kama mzigo kwa klabu hiyo kwa sababu ya mshahara wake mkubwa. ***(Gazzetta dello Sport, via Mail)***

### VARANE MIAKA MINNE
MANCHESTER United watamsajili beki wa Real Madrid na Ufaransa, Raphael Varane mwenye umri wa miaka 28 kwa mkataba wa miaka minne na uwezekano wa kuongeza mwaka mwingine mmoja. ***(Athletic)***

### TUANZEBE AWANIWA NEWCASTLe
NEWCASTLE wanapambana kukamilisha usajili wa mlinzi wa zamani wa Timu ya Taifa ya Vijana ya England chini ya miaka 21, Axel Tuanzebe mwenye miaka 23, kutoka Manchester United. ***(Telegraph)***

### WHITE RASMI ARSENAL
BEN White mwenye umri wa miaka 23 anatarajiwa kufanyiwa vipimo vya afya leo Jumatano pale Arsenal huku uhamisho wa mlinzi huyo wa England wa pauni milioni 50 ulisharidhiwa na Brighton tangu wiki iliyopita. ***(Sky Sports)***

### LUKAKU HATAKI
ROMELU Lukaku mwenye umri wa miaka 28 anafuraha kucheza Inter Milan na mshambuliaji huyo wa Ubelgiji, hana mpango wa kuondoka klabuni hapo msimu huu, licha ya Chelsea kuonyesha nia ya kumtaka ***(Express)***

### SPURS WAKOMAA NA ROMERO
KLABU ya Tottenham Hotspur imeongeza nguvu ya kujaribu kumnasa beki wa kati wa Atalanta na Argentina, Cristian Romero mwenye umri wa miaka 23, kwa ada ya pauni milioni 40. ***(Telegraph)***

### VILLA BADO KWA BAILEY
OFA ya Aston Villa ya kumsajili winga wa Bayer Leverkusen, Leon Bailey imeanza kuwa ngumu baada ya klabu za Leicester, Everton, Wolves na Southampton kuonyesha nia ya kumtaka nyota huyo mwenye umri wa miaka 23, anayepatikana kwa ada ya pauni milioni 30. ***(90min)***

### HAKUNA OFA KWA GRIEZMANN
BARCELONA hadi sasa hawajapokea ofa yoyote kwa mshambuliaji wao Mfaransa, Antoine Griezmann mwenye umri wa miaka 30. ***(Marca)***

### SHAQIRI KUTIMKA
XHERDAN Shaqiri mwenye umri wa miaka 29, anajiandaa kutimka Liverpool msimu huu, huku Napoli na Lazio ni baadhi ya klabu zilizoonyesha nia ya kutaka kumsajili winga huyo wa Uswisi. ***(Goal)***

### DJALO AWANIWA ARSENAL
ARSENAL inafikiria kumsajili winga wa Ureno, Matchoi Djalo mwenye umri wa miaka 18, kutoka Pacos de Ferreira anayepatikana kwa ada ya pauni milioni 1. ***(Sun)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# VARANE RASMI MAN UNITED

**Yakubali kulipa pauni mil. 34 huku yeye akikataa kuendelea kucheza Real Madrid...**

**MANCHESTER, ENGLAND**

MLINZI wa Real Madrid, Raphael Varane anakaribia kujiunga na Manchester United baada ya klabu hiyo kukubali kulipa ada ya awali ya pauni milioni 34 kwa usajili wake.

Makubaliano ya mwisho bado yanaendelea kufikiwa, lakini Varane mwenye umri wa miaka 28, ameiambia Real hana mpango wa kuongeza mkataba wake wa sasa, ambao umebakia mwaka mmoja.

Dili hilo la Varane linawezekana kufikia huku majadiliano zaidi yakiendelea.

Kwa mujibu wa magazeti mengi nchini Hispania na England, uhamisho wa Varane huenda ukafikia pauni milioni 42 iwapo vipengele vyote kwenye mkataba wa sasa ya beki huyo vitazingatiwa kikamilifu.

Kutua kwa Varane pale Old Trafford kutamfanya kuwa mchezaji wa pili kusajiliwa na Man United baada ya kiungo, Jadon Sancho aliyeondoka Borussia Dortmund kwa pauni milioni 73.

Varane alisajiliwa rasmi ya Real mwaka 2011 baada ya kuagana na kikosi cha Lens cha Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1.

Tangu wakati huo, ameisaidia Real Madrid kupata mataji matatu ya Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, na manne ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Alikuwa sehemu ya kikosi cha Ufaransa kilichoshinda Kombe la Dunia mwaka 2018.

Hadi sasa amecheza jumla ya mechi 79 na alicheza mara nne kwenye fainali za Euro 2020 zilizoshuhudia Ufaransa wakitolewa na Uswisi kwenye hatua ya 16 bora.

HABARI MICHEZO

## AZAM KUWATUMIA VIJANA KAGAME CUP

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Azam FC umeweka wazi kwamba, watatumia kikosi cha timu ya vijana kwenye michuano ya Kombe la Kagame, linalotarajiwa kuanza kutimua vumbi Agosti 15, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini, Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati alisema jana jioni walianza mazoezi kwa ajili ya maandalizi ya michuano hiyo.

Alisema hatua ya kuwatumia wachezaji vijana ni kwa sababu wanawapa muda wa kupumzika wachezaji wao waliocheza Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu ulioisha.

"Katika kikosi kinachokwenda kucheza kombe la Kagame, hakitakuwa na mchezaji yoyote mkubwa aliyecheza Ligi na hata wale wapya waliosajiliwa kwa ajili ya msimu ujao," alisema.

Alisema watatumia wachezaji hao kuhakikisha wanapata uzoefu wa kucheza mechi za ushindani kulingana na wengine kupata nafasi ya kupandishwa katika kikosi cha kwanza.

Azam ni miongoni mwa timu mbili ikiwamo Yanga zilizothibitisha kushiriki michuano hiyo ya kombe la Kagame na kuchezewa katika viwanja viwili Azam Complex na Benjamini Mkapa.

## MKWASA AKABIDHI RIPOTI YA USAJILI

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Ruvu Shooting, Charles Mkwasa, amesema tayari amekabidhi ripoti kwa uongozi wa timu hiyo na kuonyesha nafasi sita za usajili ikiwemo golikipa ili kuimarisha kikosi chao kwa msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Mkwasa alisema uongozi umeshaanza kufanyia kazi ripoti yake ikiwamo kutafuta mbadala wa Edward Manyama ambaye ameondoka ndani ya kikosi cha timu hiyo na kusajili na Azam FC.

"Msimu huu hatukufikia malengo yetu kutokana na kuandamwa na majeruhi, sasa nimeeleza uongozi wangu kupitia ripoti yangu kusajili wachezaji ambao wataleta ushindani na kuwepo kwa kikosi kipana na kufikia malengo yetu kwa msimu ujao," alisema Mkwasa.

Alisema umakini katika usajili unatakiwa kulingana na mipango yao ya msimu ujao kutaka kuleta ushindani mkubwa katika ligi hiyo ambayo hutarajia kuanza muda sio mrefu.

"Hatuna muda tunatakiwa kufanya kila kitu mapema, kusajili wachezaji wazuri pamoja na kuanza mapema maandalizi ya msimu, usajili utakapokamilika tunatarajia kuanza maandalizi ya msimu," alisema Mkwasa.

# SIMBA YAZOA MILIONI 100 ZA SPORTPESA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya michezo na burudani SportPesa jana imewazawadia Simba Sh. milioni 100 baada ya kushinda taji la ligi kuu Tanzania bara kwa msimu huu uliomalizika wa 2020-2021.

Hiyo ni mara ya nne mfululizo kwa Simba kujizolea fedha hizo tangu waliposaini mkataba na SportPesa kuwa wadhamini wakuu wa klabu hiyo mwaka 2017.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa kukabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 100, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya SportPesa, Tarimba Abbas, alisema: "Tukiwa kama wadhamini wakuu wa klabu ya Simba, kwa niaba ya SportPesa ningependa kuwapongeza sana kwanza kwa kuibuka mabingwa na ligi kuu Tanzania bara, pili kwa kuibuka washindi wa kombe la FA.

"Hii inatupa faraja sana kuona matunda ya SportPesa kwa klabu ya Simba tukiangalia miaka minne iliyopita tangu kuingia mkataba nao rasmi.

**Akipokea hundi hiyo, Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema kuwa anaipongeza SportPesa kwa kutimiza makubaliano yaliyokuwapo katika mkataba waliongia nao kwa kipindi cha miaka minne.**

"SportPesa wanastaili pongezi kwa kufanikiwa kutimiza makubaliano yaliyokuwepo katika mkataba ikiwemo sehemu ya bonasi. SportPesa walianza kutupa bonasi ya Sh. Milioni 50 baada ya kufanikiwa kufika hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na hii ni mara ya pili kwao kutupa Sh 100 Mil za ubingwa wa ligi."

Kwa niaba wa wachezaji, beki wa Simba, Gadiel Michael alisema kuwa "Tuchukue nafasi hii kwa kuwashukuru SportPesa kwa udhamini ambao wamekuwa wakitupa, unatupa morali, hivyo tuahidi kuendelea kupambana kwa ajili ya kuwatangaza SportPesa kimataifa.



Wachezaji wa timu ya Fedha FC ya Kivule, wakifanya usafi katika eneo la Hospitali ya Wilaya ya Ilala, Kivule jijini Dar es Salaam hivi karibuni. PICHA: JUMANNE JUMA

# Tanzania yatinga fainali CECAFA U23

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya taifa ya Tanzania chini ya miaka 23, imefanikiwa kutinga hatua ya fainali ya michuano ya Baraza la Vyama vya Soka Afrika Mashariki na Kati (CACAFA) kwa vijana chini ya miaka hiyo kwa kuichapa Sudan Kusini kwa bao 1-0 kwenye pambano kali ya nusu fainali lililochezwa Uwanja wa Bahir Dar, Addis Ababa nchini Ethiopia.

Tanzania ilibidi usubiri hadi dakika ya 65 ilipopata bao pekee kwenye mechi hiyo lililofungwa na Kelvin Nashon.

Mchezaji huyo alifunga bao hilo kutokana na mkwaju wa faulo, nje na pembeni kidogo mwa lango, mpira huo ukibabatiza mmoja wa mabeki wa timu hiyo na kujaa wavuni.

Tanzania ambayo ilikuwa Kundi A, ilifuzu kundi hilo kwa kuliongoza, ikiwa na pointi 4, ikiichapa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo bao 1-0 Julai 21, kabla ya kutoka sare ya bao 1-1 na Uganda na kufanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali.

Fainali hiyo itachezwa Jumamosi kusaka bingwa na michuano hiyo.

# Michezo

Jumatano Julai 28, 2021


Nipashe





## Varane rasmi Man United

HABARI UK. 22




Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi SportPesa, Tarimba Abbas (kulia) akimkabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 100 Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbra Gonzalez, mbele ya wachezaji Beno Kakolanya na Gadiel Michael, ikiwa kama bonasi ya timu kwa kuchukua ubingwa na Ligi Kuu Tanzania Bara. **PICHA; MPIGAPICHA WETU**

# SIMBA: HATUJAPATA OFA YA MIQUISSONE

### ●●●Mangungu asema hakuna mchezaji atayeondoka, Try Again adai wao wanafanya biashara wako...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Simba imesema haijapata ofa toka kwenye klabu yoyote inayomhitaji mchezaji wake, Luis Miquissone raia wa Msumbiji.

Mwenyekiti wa Simba, Murtaza Mangungu amesema kuwa hakuna mchezaji atakayeondoka mpaka pale watakapokaa na benchi la ufundi kuangalia ni vipi wakisuke tena kikosi chao cha msimu ujao kiwe tishio kuliko msimu huu, ndipo mengine yafuate.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya klabu hiyo, Salim Abdallah 'Try Again', yeye amesema kuwa habari hizo ambazo zimeenea kila kona nchini na hata nje ya mipaka ya Tanzania, hazina ukweli kwa sababu hakuna klabu yoyote iliyokuja kwao kumtaka mchezaji huyo.

"Mezani hakuna kitu kama hicho. Hatujapata ofa yoyote ya klabu yoyote kumtaka mchezaji wetu Luis," alisema Try Again.

Hata hivyo, alisema iwapo kuna klabu yoyote inamhitaji wao wako tayari kumuuza kwa sababu pamoja na soka, lakini wanafanya biashara.

"Kama kuna timu inamhitaji ije tu. Sisi tunafanya biashara na hatumzuii mchezaji. Mwenye uwezo aje, hakuna tatizo," alisema kiongozi huyo.

Kwa upande wake Mangungu alisema watalisikiliza benchi la ufundi kwanza baada ya mashindano kumalizika.

"Hatuwezi kusema lolote kwa sasa. Kwanza tutalisikiliza benchi la ufundi lituambie sehemu gani kuna mapungufu, nani atoke, nani abaki, nani aingie, ndipo tunapoweza sasa kutoka na kuzungumza nini kimefanyika," alisema.

Klabu mbalimbali zilizocheza Ligi ya Mabingwa Afrika zinatajwa kumwania mchezaji huyo machachari zikiwamo Kaizer Chiefs ya Afrika Kusini na Al Ahly ya Misri.

Hata hivyo, tetesi zinaitaja klabu ya Al Ahly ndiyo imeonekana kumhitaji zaidi kutokana na uwepo kwa kocha, Pitso Mosimane ambaye ameshawahi kumfundisha mchezaji huyo akiwa Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini.

Viongozi hao wa Simba kila mmoja alisema kuwa baada ya msimu wao kumalizika ukiwa wa mafanikio, wanatarajia kukisuka tena kikosi chao kwenye baadhi ya maeneo ili kuendelee kuwa cha kutisha barani Afrika, achilia mbali Ligi Kuu ya Tanzania kwa msimu ujao.

## Nabi atwaa tuzo, Mugalu mchezaji bora

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi ametwaa tuzo ya kocha bora wa Julai, huku mshambuliaji wa Simba, Chris Mugalu akichaguliwa kuwa mchezaji bora wa mwezi huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo ilimalizika Julai 18.

Taarifa iliyotolewa jana na Bodi ya Ligi, Nabi na Mugalu ndio waliong'ara kwa mwezi huo.

Nabi, aliisaidia Yanga kushinda mechi mbili za Julai, ikiwafunga Ihefu FC na Simba, huku ikitoka suluhu na Dodoma Jiji.

Kocha huyo alijiunga na Yanga Aprili baada ya klabu hiyo kumtimua Cedric Kaze na tangu atue amekuwa msaada mkubwa wa kikosi hicho hadi kumaliza ikiwa kwenye nafasi ya pili.

Mugalu amechaguliwa kuwa mchezaji bora wa mwezi huo baada ya kuwashinda Charles Ilamfya wa KMC na Juma Luzio wa Mbeya City.

**Mchezaji huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Kongo (DRC), aliyesajiliwa na Simba msimu huu akitokea Power Dynamos ya Zambia, alifunga mabao matano mwezi huo akiisaidia Simba kushinda mechi tatu na ikapoteza moja.**

Wachezaji ambao wamechukua tuzo kwa msimu huu ni Prince Dube wa Azam, Septemba, Mukoko Tonombe wa Yanga, Oktoba, John Bocco wa Simba, Novemba, Saido Ntibazonkiza wa Yanga, Desemba, na Deogratius Mafie wa Biashara United, Januari.

Wengine ni Anuary Jabir wa Dodoma Jiji, Februari, Luis Miquissone wa Simba, Machi, Claotus Chama pia wa Simba, Aprili.

Dude alirudia tena Mei, huku Bocco akiibeba pia Juni.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >